epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Ijumaa Septemba 27, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581812
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital




UKURASA WA 22

**MBAPPE MAJANGA REAL MADRID**

KLABU ya Real Madrid imetangaza mshambuliaji wake nyota wa kimataifa wa Ufaransa, Kylian Mbappe amepata majeraha na atakuwa nje kwa...

UKURASA WA 2

**Samia** aorodhesha mikakati kukabili wanyamapori wavamizi vijijini

UKURASA WA 4

**Polisi** yajibu TLS: Hatusubiri moto uwake ilhali moshi unafuka



UKURASA WA 3

**Utafiti** wabaini uhusiano kati ya darasani na afya ya akili

# Ana miaka 13 tayari ni mama

• **Baba** wa mtoto ni kaka yake... *Endelea ukurasa 8*



## Wasota saa 4 majini boti ikizama, wawili wafa

UKURASA 3



Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Ilemela, mkoani Mwanza (wa pili kushoto), Deusdedith Rutta akiteta jambo na mmoja wa askari wa jeshi hilo, baada ya kutoka katika eneo ilipotokea ajali ya boti ya MV. Sea Falcon, kwenye Ziwa Victoria jana, kwa ajili ya uokoaji. **Picha ndogo:** Muuguzi Kiongozi wa wodi ya wanaume ya Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza Sekou Toure, Roza Nkeso (katikati) akishirikiana na Muuguzi Msaidizi, kumhudumia mmoja wa majeruhi wa ajali hiyo. **PICHA: VITUS AUDAX**

**MICHEZO** **GAMONDI: SOKOINE IMETUNYIMA MABAO** UK.24 **KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Majaliwa ataka ushirikiano utekelezaji uchumi jumuishi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa wito kwa wadau wa maendeleo kushirikiana kikamilifu na nchi zinazoendelea katika kusaidia utekelezaji wa mifumo jumuishi ya kifedha.

Majaliwa alitoa wito huo juzi wakati akifungua mjadala kuhusu miaka 15 ya mafanikio katika Mfumo Jumuishi wa Fedha kwa Maendeleo kwenye mkutano ulioitishwa na Malkia wa Uholanzi, Maxima, ambaye ni Mwakilishi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika Huduma Jumuishi za Fedha, New York, Marekani.

Alisema uchumi jumuishi ni muhimu hasa katika utekelezaji wa mpango endelevu wa maendeleo na ufanikishaji wa ajenda 2030.

"Huduma jumuishi za kifedha ni kiungo muhimu cha ukuaji wa uchumi, kupunguza umasikini na kuleta maendeleo ya jamii kwa ujumla," alisema Waziri Mkuu.

Aidha, Majaliwa alimpongeza Malkia Maxima kwa juhudi ambazo zimewezesha ongezeko kubwa la kufikiwa kwa huduma za kifedha duniani, huku zaidi ya asilimia 50 ya watu wakiwa wamefikiwa na mpango huo katika kipindi cha muongo mmoja uliopita.

"Umiliki wa akaunti duniani umeongezeka kutoka asilimia 51 mwaka 2011 hadi kufikia asilimia 76 mwaka 2021. Haya ni mafanikio makubwa lakini changamoto imebaki hasa kwa wanawake waishio katika nchi zinazoendelea. Wengi wao bado hawajaingizwa kwenye mfumo jumuishi wa kifedha," alisema.

Awali, Malkia Maxima alisema anafurahishwa na hatua iliyofikiwa sasa ikilinganishwa na hali ilivyokuwa hapo awali.

"Wakati tunaanza hii kazi ya kuhimiza mifumo jumuishi ya kifedha hatukuwa na takwimu zozote. Tulipanda na kufikia asilimia 50 na sasa tunakaribia asilimia 80. Natambua asilimia 80 siyo sawa na asilimia 100, ni lazima nikiri kuwa kazi imefanyika," alisema.

Akionesha dhahiri kuwa bado kazi haijaisha, Malkia Maxima alisema mkakati uliopo ni kuwafikia watu bilioni 1.5 ambao bado hawajafikiwa na huduma jumuishi za kifedha.

Alisema anafarijika kuona watu wa rika mbalimbali wakitumia mifumo hii kwenye maeneo ambayo huduma za kifedha zinapatikana.

"Mabibi wanaweka fedha na kusomesha wajukuu zao, vijana na mabinti wajasiriamali wanatumia huduma hizo kutunza fedha zao, kupata mikopo midogo midogo na kukuza mitaji yao," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aliishukuru serikali ya Marekani kwa misaada inayoipatia Tanzania kupitia wadau mbalimbali kama Shirika la Misaada ya maendeleo (USAID), Vodafone Foundation, Rockefeller Foundation na Ford Foundation na hasa kwenye masuala ya uchumi, kijamii na utawala bora.

Alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anashukuru kwa hatua hiyo kwani inaendana na maboresho ambayo serikali yake imeamua kuyatekeleza ili kuleta ujumuishi kwenye jamii kwa faida ya siku za usoni.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA DAR ES SALAAM

SHAURI LA UTEKELEZAJI NA. 16686 YA MWAKA 2024

THE REGISTERED TRUSTEE OF COMMUNITY .................... 1 MUOMBAJI
DEVELOPMENT TRUST FUND ..........................................2 MUOMBAJI

*DHIDI YA*

HUBERT HENRY SANGU & NATIONAL BANK OF
COMMERCE LIMITED..........................................................MDAIWA

KWA:

Hubert Henry Sangu,
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa mwombaji aliyetajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati ya Madai zinazopatikana katika Mahakama hii, unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii, wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 02/10/2024 saa tatu (3:00) asubuhi mbele ya Mhe. **A.H.Mbadjo** Kwa ajili ya Hukumu.

**ANGALIA:**

Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikathibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.

**HATI** hii imetolewa kwa **MKONO** wangu na **CHAPA** ya Mahakama leo hii tarehe 19 Mwezi Septemba, 2024.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwasalimia wananchi wa Kata ya Mchomoro, Wilaya ya Namtumbo, mkoani Ruvuma jana. **PICHA: IKULU**

# Samia aorodhesha mikakati kukabili wanyamapori wavamizi

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali imeanza kuchukua hatua za kukabiliana na wanyamapori waharibifu wanaovamia mashamba ya wananchi na kuharibu mazao wakiwamo tembo.

Ametaja moja ya mpango ni kuongeza ndege nyuki na kuimarisha vituo vya askari wa maliasili ili kurahisisha kazi ya kuwadhibiti.

Akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Tunduru kwa nyakati tofauti ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya siku ya nne Mkoa wa Ruvuma, Rais Samia pia amezindua soko la madini Tunduru.

Rais Samia alitaja mikakati inayofanyika kuwa ni pamoja na kuongeza askari wa wanyamapori katika maeneo mbalimbali na kuwaongezea ujuzi askari wanyamapori wa vijiji ili washirikiane kuwadhibiti.

Alisema serikali imeweka magari ya doria katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo yanayorahisisha utekelezaji wa shughuli hiyo pamoja na ndege nyuki inayotumika kufukuza tembo.

"Tunajua kuna tatizo la tembo, lakini tumeanza kuchukua jitihada hizo na mengine yanafuatia, lengo letu ni kuongeza idadi ya ndege nyuki ili kufukuza tembo na kuimarisha vituo vya askari wa maliasili ili waweze kufanya kazi ya kuwafukuza," alisema Rais Samia.

Rais Samia alisema serikali inaendelea kuwashika mkono wakulima kwa kutoa ruzuku na kuongeza bei ya kununua mazao hadi kufikia Sh. 700 kwa kilo, ili kukuza sekta ya kilimo na kuwasisitiza kuongeza uzalishaji wa mazao.

Alimwagiza Waziri wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo kushirikiana na Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, kuhakikisha wanafufua kiwanda cha kubangua korosho kilichoko wilayani humo na kukitafutia mwekezaji mwingine baada ya yule wa zamani kushindwa kukiendesha.

"Tunataka kilimo kikue, kichangie katika pato la taifa, kwa kiasi kikubwa na tunauona mwelekeo.

Kwa hiyo niwaombe sana ndugu zangu wananchi tufanye kazi kwa bidii," alisisitiza.

Aliwaonya wakazi wa eneo hilo kuacha kuchoma moto mashamba, kwa kuwa kunasababisha uharibifu wa mazingira ikiwamo misitu, barabara na kuharibu taswira ya nchi na kuchochea athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Mkichoma moto mnaharibu misitu, lami ile ikipata moto inayeyuka barabara zinaharibika, sasa badala ya kuwaletea maendeleo pesa ileile inarudi tena kutengeneza barabara, tukaimarishe misitu inakuwa kazi kubwa.

"Eti nani aliwaambia kuwa ukichoma moto eneo kubwa ndio baraka ya biashara, haya mlishachoma moto, mlipata hiyo biashara? Basi acheni kuchoma moto," aliagiza.

Aliwaagiza viongozi wa wilaya hiyo kuhakikisha kuwa wanadhibiti uchomaji wa mashamba ovyo na kuhakikisha kuwa mazingira yanatunzwa ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi na kukuza kilimo.

Alisema kuwapo soko la madini kutawahakikishia wachimbaji wadogo bei nzuri ya bidhaa hiyo kutokana na ushindani utakaokuwapo.

Aliwaagiza viongozi wa wilaya hiyo kama wanaona kuwa kuna haja ya kujenga soko lingine, wazungumze na sekta binafsi ili lijengwe kwa njia ya ushirikiano.

Aliwakumbusha vijana na wanawake kujitokeza kwa wingi kujiandikisha na kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao na kuchagua viongozi wanaowakilisha maslahi yao.

Alisema serikali itajenga hosteli za kukaa wanafunzi wasichana katika Jimbo la Tunduru Kaskazini kama mbunge wake, Hassan Kungu, alivyoomba.

Awali, Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, Vita Kawawa, alimwomba Rais Samia katika kuzuia usumbufu wa wanyamapori waharibifu ambao wamekuwa akivamia mashamba ya wanakijiji na kuharibu mazao, juhudi za kuwadhibiti ziongezwe.

Mbunge wa Tunduru Kusini, Idd Mpakate, alimwomba Rais Samia awasaidie kugawanya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, ili kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya utawala wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Tunduru, Chiza Marando, alisema Soko la Madini, limejengwa kwa ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi na ujenzi wake umegharimu Sh. bilioni 1.4.

Alisema kati ya hizo fedha, wafanyabiashara wa madini wamechangia Sh. bilioni 1.085 na Halmashauria Sh.milioni 319. Kati ya fedha hizo Sh. milioni 288 ni thamani ya ardhi ya eneo lilijengwa jengo hilo.

Alisema ujenzi wa soko hilo utasaidia kudhibiti utoroshaji wa madini kwa sababu lina vyumba vya kutosha kuweka wafanyabiashara wote katika eneo moja.

# DC ahimiza stadi za maisha shuleni

**Na Agustino Kihombo,** IRINGA

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Kheri James, amewataka walimu kurejesha somo la stadi za kazi kwa wanafunzi zikiwamo kilimo, mapishi na mambo ambayo yatasaidia kuwaandaa kujitegemea pindi watakapohitimu masomo.

James alitoa agizo akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika wilaya ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule mbalimbali za msingi na sekondari yenye lengo la kuboresha mazingira ya utoaji elimu kwa watoto na kuongeza ufaulu.

Aliwakumbusha walimu wajibu wa kufundisha masomo ya stadi za kazi ikiwamo kilimo kujitambua ili kuwaandaa na maisha ya baadaye kwa kuwa vijana wasiowajibika ni mzigo kwa taifa na jamii kwa jumla.

"Niwapongeze walimu kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kufundisha na kuhakikisha wanafunzi wanafaulu mitiahani. Lakini niwakumbushe kufundisha darasani pekee haitoshi kuwaandaa watoto kuwa na maisha ya kujitegemea baada ya kuhitimu.

"Kwa hiyo ni muda sasa wa kuanza kufundisha stadi za kazi kama kilimo. Hii itamfanya mwanafunzi kujitambua na kuwa mtu mzuri, hivyo kuwa na uwezo wa kujitegemea," alisema.

Kuhusu malezi, James alisema sehemu salama kwa mtoto ni shuleni na kwenye familia kwa hiyo kuna haja kwa walimu kuwa mfano wa kuigwa na wanafunzi nje ya masomo wanayofundisha, ikiwa na maana matendo watakayoyafanya yawe kielelezo kwa wananfunzi wawapo shuleni .

Suala la stadi za kazi linafanya na baadhi ya shule ikiwamo Shule ya Msingi Kalenga ambayo ina mkakati wa kutumia mashamba ya shule kuzalisha mazao. Jamii imeamua kutumia mashamba hayo kulima mazao kwa ajili ya chakula cha wanafunzi lakini pia yatumike kama shamba darasa kwa wananfunzi kujifunza shughuli za kilimo ili kuwaandaa na maisha ya baadaye.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Shaibu Mingaula, alisema kwa kushirikiana wananchi wa kijiji cha kalenga, wametenga zaidi ya ekari 40 kwa ajili ya kilimo kujihakikishia usalama wa chakula shuleni na kutumia shamba hilo kama shamba darasa la kufudishia watoto stadi za kazi.

"katika kutekeleza azma ya serikali ya kuwapa watoto chakula, kamati ya shule kwa kushirikiana na wazazi, iliamua kuwasilisha wazo kwa serikali ya kijiji ili kuwe na shamba la shule ambalo litahudumiwa na wananchi wenyewe.

Mpaka sasa tumefanikiwa kulima kwa msimu mmoja na tunaendelea kujipanga kwa ajili ya msimu wa kilimo ujao. Tumejipanga kulima mahindi na maharage ili kuwa na uhakika wa chakula shuleni," alisema.

Baadhi ya wazazi na wananchi wa kijiji cha Kalenga, wakiwamo Elmina Mgongolwa na Georgina Mhavile, walisema walikubaliana kuwa na shamba la shule ili kupunguza michango ambayo ilikuwa inasababisha watoto ambao wameshindwa kuchangia kutokula chakula wawapo shuleni.

Nae Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Steven Mhapa, aliyeambatana na Mkuu wa Wilaya katika ziara hiyo, alisema mkakati wa halmashauri wa kuhakikisha shule zote zinakuwa na mpango wa chakula shuleni ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi na tayari maelekezo yametolewa kwa walimu kusimamia mpango huo.




Naibu Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania, Melisa Mc-Neil- Barrett, akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Uzazi wa Mpango, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: SABATO KASIKA**

# Utafiti wabaini uhusiano uelewa wa mtoto darasani na afya ya akili

**Na Christina Mwakangale**

UTAFITI umebaini kuwapo kwa uhusiano mkubwa kati ya uelewa darasani na afya ya akili kwa watoto walio katika umri wa madarasa ya awali.

Kwa mujibu wa utafiti huo, asilimia 41 ya watoto wamebainika kuwa na tatizo la akili, hivyo kushindwa kumudu mbinu za kusoma na kufaulu.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE) Dk. Nabwera Rashid, aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha matokeo ya utafiti alioufanya kuhusu Afya ya Akili ya Watoto wa Shule ya Awali na Uhusiano kwenye Matokeo ya Masomo ya Awali nchini.

Mhadhiri huyo wa chuo hicho kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), akizungumza kwa njia ya mtandao kuhusu utafiti huo uliondaliwa na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kupitia Jumuiya ya Wadau wa Afya ya Akili Tanzania (TMH-CoP) ECHO, alisema afya ya akili utotoni inahusisha ustawi wa kihisia, kijamii na kisaikolojia wa watoto wenye umri wa miaka sifuri hadi mitano.

Utafiti alioufanya kwa kuhusisha wilaya tatu za Arumeru mkoani Arusha, Kinondoni (Dar es Salaam) na Nzega (Tabora), ulihusisha watoto 403 wa umri wa miaka sifuri hadi saba, wakiwamo wa kike ambao ni asilimia 49.6.

Alisema utafiti ulibaini kuwa kati ya watoto hao waliohusishwa kwenye utafiti ambao ni 403, baadhi wakiwa madarasa ya awali kwa madaraja tofauti, ilibainika watoto 169 sawa na asilimia 41, hawako sawa katika afya ya akili, hivyo kuathiri mwenendo wa ujifunzaji.

Dk. Nabwera alitaja maeneo ambayo watoto hao huathirika zaidi ni katika kuelewa hatua za kusoma kama vile ufahamu wa fonimu, kutaja majina ya picha, ujuzi wa msamiati na ufahamu wa fonetiki.

"Watoto watundu wanaosababisha matatizo kadhaa 131 ya waliohusishwa kwenye utafiti, hasa nilibaini watoto ni watundu sana yaani hawatulii hata darasani, kwa sababu Dar es Salaam (Kinondoni) ni miongoni mwa mikoa ambayo wazazi, walezi wako 'bize' hawana muda wa kulea hawa watoto. Katika kila watoto 10 unaokutana nao njiani watatu hadi watano, wana tatizo la akili.

Matokeo yalionesha kuwa asilimia 58 ambao ni sawa na watoto 235 wa shule ya awali, walikuwa na alama chini ya wastani katika mtihani wa ujuzi wa kusoma Kiswahili.

"Hii ina maana kwamba watoto wengi wa shule ya awali, hawakuwa na ujuzi wa kutaja alfabeti, sauti za alfabeti, kusoma na kuelewa, kushika na kufungua vitabu, utambulisho wa barua, majina ya picha na kadhalika.

"Mara nyingi mijadala huhusu afya ya akili inahusu vijana, sasa huu utafiti melenga watoto. Umri huu mtoto hujaribu ku-handle hisia zake na masuala mengine ya kijamii. Huu ndio umri wa kuanza shule, kuna haja ya watoto wa umri huo, kufuatiliwa uweao wao wa uelewa, kuhusiana na jamii nkwa kuwa nao afya ya akili huathiriwa.

Watoto wengi umri huu, ndio wanaingia elimu ya awali, wanafundishwa kusalimia, kuwa na marafiki, kunawa mikono na aseme asante, au samahani na asipopata elimu hii ndio utakutana na watu ukubwani yeye hana hisia zozote za shukrani, kuomba radhi wala huzuni," alisema.

Kwa mujibu wa utafiti huo, asilimia 2.8 watoto wa umri huo wako darasani kwa madaraja tofauti kuanzia elimu ya awali. Katika kila darasa, watoto 10 hadi watano wana tatizo la akili.

"Uchokozi, wizi, uongo, hasira hadi anajipiga chini, nyuma yake kuna tatizo la akili na mzazi au jamii bado hajatambua. Labda akiwa darasani unamwambia nenda mbele kasome au nenda kalale hatekelezi ujue kuna shida. "Utakuta mtoto anamaliza kula anatupa sahani hadi inavunjika au akila hapeleki sahani inakotakiwa, ujue kuna shida. Anayefanya vizuri ujue ameshaanza kujua 'social interactions' kwamba huyu mkubwa, huyu mdogo," alibainisha.

Mhadhiri huyo alisema mtoto aliye na afya ya akili duni akiwa katika umri wa chini ya miaka mitano, akifikia umri wa miaka 14 tatizo litakua.

"Kwa Dar es Salaam, tatizo la watoto watundu ni kubwa kwa sababu wazazi wanakimbizana kutafuta maisha. Hii inaweza kuathiri jamii ya kesho, hawa ndio wazazi na wanajamii wajao miaka 10 hadi 20 ijayo,"alisema Dk. Nabwera.

Alisema elimu ya afya kwa watoto hao ni muhimu kutokana na watoto kujumuisha theluthi moja ya watu wote duniani na asilimia 40 kati yao wanaishi barani Afrika, kwa mujibu wa Shirika la Idadi ya Watu la Umoja wa Mataifa mwaka 2022.

Shirika la Afya duniani (WHO) linakadiria kuwa asilimia 10 hadi 20 ya watoto na vijana hupata changamoto ya akili kwa maana kwamba katika kila watoto 10 kutoka miaka mitatu hadi 12, watatu hadi watano wana tatizo la akili huku zaidi ya asilimia 90 ya kesi hizo zikitokea katika nchi za kipato cha chini na kati kama Tanzania.

Nchini Tanzania, ni asilimia 2.8 tu ya watoto wenye umri wa miaka mitatu hadi sita wanahudhuria shule ya awali, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) ya mwaka 2020.

Takwimu za hivi karibuni kimataifa, zinaonesha katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, takribani watoto milioni 202 wenye umri wa miaka minne hadi 14 hawawezi kusoma kwa ustadi baada ya kuhitimu.

Nchini Tanzania ni asilimia 12 tu ya wanafunzi wa darasa la pili wanaokidhi viwango vya ufasaha vya kitaifa vya usomaji wa sauti 50 kwa dakika katika Kiswahili.

# Polisi hatutasubiri moshi ufuke kuchukua hatua uvunjifu amani

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini limesema kamwe halitasubiri kuona moto ndipo lichukue hatua ilhali moshi unafuka kuashiria vitendo vya uvunjifu wa amani.

Limesisitiza kwamba litaendelea kuchukua hatua stahiki kwa mtu, watu au kikundi cha watu, kiongozi wa chama cha siasa au wafuasi wao wanaopanga, wanaohamasisha au wanaotenda vitendo vya kihalifu vinavyoweza kusababisha uvunjifu wa amani.

Kauli hiyo imetolea baada ya watu na makundi mbalimbali, akiwamo Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Wakili Boniphace Mwabukusi, kusema kuwa Jeshi la Polisi halina mamlaka ya kuzuia maandamano ya vyama vya siasa.

Wadau hao wamesema wajibu wa jeshi hilo ni kuyasimamia na kuyasindikiza kuhakikisha kuwa yanafanyika kikamilifu.

Akijibu hoja hiyo jana, Msemaji wa Jeshi hilo, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) David Misime alisema: "Jeshi la Polisi litaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 5 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi kama ilivyorejewa mwaka 2002, ikiwamo kulinda amani ya nchi."

DCP Misime alisema katika maoni ya wadau hao, wametaja vifungu vya sheria ikiwamo vifungu vya 11 (7) na (8) vya Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura 258, kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Alisema kuwa wadau hao wamesema Jeshi la Polisi limeshindwa kutoa sababu za kisheria za kuzuia maandamano ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

"Kwamba limeshindwa kusema ni lini maandamano yanaweza kufanyika baada ya zuio na kuongeza kuwa Jeshi la Polisi halikutakiwa kuingilia masuala ya vyama vya siasa kwa sababu wajibu huo upo kwa Msajili wa Vyama vya Siasa.

"Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura 258, kifungu cha 11 (7) (c), inaeleza kuwa endapo mkutano au maandamano yanaonesha au yamedhamiriwa kusababisha uvunjifu wa amani au kuathiri usalama wa umma katika eneo hilo, Mkuu wa Polisi ambaye amepokea taarifa ya mkutano au maandamano hayo atatoa zuio la kufanyika kwa mkutano au maandamano hayo kwa mujibu wa kifungu cha 11 (6) cha sheria hiyo.

"Kifungu cha 11 (8) cha Sheria ya Vyama vya Siasa kinasema ni sharti zuio liwe kwa maandishi na litoe sababu za zuio hilo," alisema.

DCP Misime alisema kuwa katika kutekeleza kifungu hicho, sharti la kutoa sababu za kuzuia maandamano hayo lilitekelezwa na maofisa ambao walipokea taarifa za kufanya maandamano na sababu zilizoainishwa ni pamoja na matamshi kutoka kwa viongozi na wafuasi wa chama kilichowasilisha taarifa ambayo yalikuwa na viashiria vya wazi vya kuvuruga amani ya nchi.

"Kuhusu kutoa taarifa ya lini maandamano hayo yafanyike, sheria haimlazimishi Mkuu wa Polisi anayetoa zuio kueleza ni lini mkutano au maandamano yaliyozuiwa yanaweza kufanyika," alidai.

Alisema kuwa mujibu wa Katiba Sura ya 2 ya mwaka 1977 ibara ya 20 (1) ikisomwa pamoja na Sheria ya Vyama Vya Siasa Kifungu cha 11(1)(a) na Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Kifungu cha 43 (1) (a), (b) na (c), vinatoa haki ya kufanya mikutano au maandamano katika eneo lolote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hata hivyo, DCP Misime alisema pamoja na sheria hizo, Jeshi la Polisi linawaelimisha wananchi kuwa ili kuelewa vyema masuala ya kisheria ni vyema kusoma sheria husika sambamba na sheria zingine zinazohusiana na jambo husika.

"Pamoja na haki zilizotolewa na Katiba na sheria zingine, watambue kuwa hakuna haki isiyokuwa na wajibu kama inavyoainishwa na Ibara ya 30 ya Katiba Sura ya 2 ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na Kifungu cha 11(6) na (7) cha Sheria ya Vyama vya Siasa na Kifungu cha 43 (3) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, ambazo zinatoa mipaka kwa haki na uhuru na hifadhi kwa haki na wajibu," alisema.

DCP Misime aliwataka wananchi kufahamu kuwa sheria hiyo imeeleza endapo chama cha siasa kitawasilisha taarifa ya kufanya mkutano au maandamano na Ofisa wa Polisi wa eneo husika akawaandikia barua ya kuzuia mkutano au maandamano hayo, kwa mujibu wa Kifungu cha 43(6) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, kinaelekeza chama husika kukata rufani kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi," alisema.



Naibu Waziri Mkuu, Doto Biteko (kulia), akipata maelezo uchakataji wa kahawa kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wadau wa Kahawa wa Sekta Binafsi katika nchi 11 Barani Afrika, Amir Esmail (wa pili kushoto), alipotembelea Maonesho ya Kimataifa ya Viwanda Tanzania TimeXpo 2024, katika viwanja vya Sabasaba Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wasota saa 4 majini boti ikizama, 30 wanusurika, wawili wafariki

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya abiria walionusurika katika ajali ya boti ya mizigo MV. Sea Falcon iliyolazimisha kubeba zaidi ya abiria 30 kutoka Kirumba, mkoani Mwanza kwenda kisiwani Goziba, mkoani Kagera, wamesema boti ilianza kuzama saa 12 jioni, wakapata msaada saa nne usiku.

Ajali ya boti hiyo iliyosajili MTZ 012212 ilitokea juzi katika Ziwa Victoria, Km mbili kutoka Mwalo wa Bwiru, wilayani Ilemela, mkoani Mwanza.

Wakisimulia kwa nyakati tofauti jana wakati wakiendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza (Sekou Toure), manusura hao walisema walikunywa mafuta ya petroli yaliyokuwa yakimwagika kutoka mapipa waliyoshikilia kujiokoa.

Mfanyabiashara na Mkazi wa Mbagala, Dar es Salaam, Noris Mwene, alisema kuwa baada ya kuanza safari umbali wa zaidi ya Km moja, boti hiyo ilianza kuingiza maji ndani na kuanza kuzama majira ya saa 12 jioni.

"Baada ya kuanza kujaa maji, nahodha pamoja na msaidizi wake walituambia wanahitaji kurejesha boti hiyo nchikavu kwani kuna kitu ambacho walikisahau lakini baadaye wakashauriana waendelee na safari licha ya kuonekana boti inaendelea kujaa maji," alisema. Aliendelea kusimulia kuwa baada ya muda mfupi, boti hiyo ilianza kuzama; wakamwaga mafuta yaliyokuwa kwenye mapipa ili kuwasaidia kuelea kutokana na kukosa msaada.

"Hali hiyo iliendelea hivyo mpaka majira ya saa nne usiku, walifika baadhi ya wavuvi na kutusaidia.

"Awali walikuja baadhi ya wavuvi wakakuta tunaendelea kuelea, tulipowaomba msaada walichukua tu mizigo yetu, yakiwamo mapipa ya mafuta pamoja na fedha tulizokuwa nazo kisha kuondoka bila kutupatia msaada wa aina yoyote huku mapipa yale ya mafuta yakiendelea kutupiga usoni na kunywa petroli iliyokuwa ndani ya mapipa hayo," alisema.

Alisema kuwa yey alikuwa wa kwanza kupata msaada majira ya saa tatu na nusu usiku, akisaidiwa na vijana waliokuwa na mitumbwi midogo.

"Nilipofika nchikavu nilianza kuwatafutia msaada na kumpata mwenyekiti wa eneo hilo aliyenisaidia kupata mawasiliano ya Jeshi la Polisi pamoja na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji waliofika majira ya saa nne na kuanza kushirikiana na wavuvi wengine walikuwa wakiendelea kuokoa watu," alisimulia.

Lucia Kubagwa, mfanyabiashara na Mkazi wa Nyarugusu, mkoani Geita alisema walifika bandarini Kirumba na kukuta tayari boti ya abiria imeondoka, hivyo wakaambiwa kuwa hata hiyo ilikuwa inaelekea huko na kuwa inabeba abiria. Waliaminishwa kuwa zaidi ya abiria 40 wanaweza kuingia katika boti hiyo.

"Tulipiga kelele sana bila msaada, tukaanza kumwaga mafuta ya petroli na kuelea katika mapipa hayo huku tukinywa mafuta yaliyokuwamo ambayo mpaka sasa ninajihisi tumbo na kifua vinauma kutokana na mafuta hayo niliyokunywa," alisema Lucia.

Akizungumza katika eneo la tukio, shuhuda wa tukio hilo ambaye pia ni mmiliki wa eneo la mwalo walikokuwa wakipokewa majeruhi hao, Joseph Masole, alisema ajali hiyo ilitokea Km mbili kutoka nchikavu ambako baada ya mmoja wa abiria kufika nchikavu walianza kushirikiana naye kupeleka mitumbwi ili kutoa msaada wa uokoaji.

"Alifika anasema tupo watu kama 60 tunahitaji msaada, nikatuma mitumbwi ikaenda kuokoa watu na wakati huo tukiendelea na kuomba msaada kutoka vyombo vya ulinzi na usalama. Magari ya wagonjwa yaliletwa kwa ajili ya kuwapokea wote waliokuwa wakiokolewa," alisema Masole.

Akizungumza hospitalini huko, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza (Sekou Toure), Bahati Msaki alisema usiku wa kuamkia jana alipokea mwili wa mtoto wa kiume Kharidi Rajabu (6) na Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Goziba, wilayani Muleba.

Pia alisema walipokea majeruhi 28. Kati yao, 22 wanaume na wanane wanawake ambako hadi kufikia jana majeruhi 14 walikuwa wameruhusiwa huku wengine 14 wakiendelea kupatiwa matibabu.

Jeshi la Polisi mkoani Mwanza kupitia Kamanda wa Polisi Mkoa huo, DCP Wilbrod Mutafungwa, lilithibitisha kuwakamata watu watatu, akiwamo mmiliki wa boti hiyo, Amon Lutabanzibwa kutokana na kulazimisha kutumia boti hiyo kubeba abiria bila kuwa na kibali cha kufanya kazi hiyo kutoka Shirika la Uwakala wa Meli nchini (TASAC).

Kamanda Mutafungwa alitaja wengine waliokamatwa kutokana na ajali hiyo kuwa ni pamoja na Robert Kabota (31), nahodha wa boti hiyo na Salum Shaban (59), msimamizi wa boti hiyo ambao wote wanaendelea kuhojiwa kuhusu ukiukwaji sheria za usafirishaji majini.

"Walionusurika ni watu 30 kati ya 32 kwa idadi tuliyonayo ambako pamoja na mtoto huyo aliyefariki dunia na mtu mwingine ambaye hajajulikana jina na alikuwapo katika ajali hiyo, bado tunamtafuta," alisema DCP Mutafungwa.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda alisema serikali itagharamia matibabu ya majeruhi wote na kuwataka ndugu wa baadhi ya watu ambao hawajapatikana kuendelea kuwa wavumilivu wakati vyombo vya usalama vikiendelea kufuatilia.

**HABARI KITAIFA**



Makamu Mwenyekiti wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam, Tausi Msangi akizungumza wakati wa kuunda uongozi wa watoto wa eneo hilo juzi, utakaoshirikiana na kituo hicho katika vita dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Walioshtakiwa kubaka kwa kundi waanza kujitetea

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WASHTAKIWA wanne wa kesi ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya, jijini Dar es Saalam, wameanza kutoa utetezi mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma.

Walioanza kutoa utetezi wao juzi ni pamoja na mshtakiwa namba moja ambaye ni Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Clinton Damas, maarufu Nyundo na Amin Lema, maarufu Kindamba.

Akizungumza nje ya mahakama, Wakili wa Washtakiwa hao, Meshack Ngamando, alidai kuwa siku ya kwanza, wamefanikiwa kuleta mashahidi wawili.

"Leo (juzi) hawa wawili ndio wametoa utetezi wao mbele ya mahakama, lakini tunao jumla ya mashahidi 10 ambao tunatarajia wote kesho (jana) watatoa ushahidi wao," alisema.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma iliwakuta na kesi ya kujibu washtakiwa hao wanne kwa kesi ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti huyo.

Upande wa Jamhuri ulileta jumla ya vielelezo 12 na mashahidi 18 ambao walitoa ushahidi kuhusu kesi inayowakabili washtakiwa wanne.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Askari Magereza Praygod Mushi na Nickson Jackson, maarufu Machuche.

Agosti 19 mwaka huu, washtakiwa hao wanne walifikishwa katika mahakama hiyo wakikabiliwa na makosa mawili, likiwamo la kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume na maumbile binti huyo.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Zabibu Mpangule.

Ikiwa watathibitika kutenda kosa hilo, adhabu yake ni kifungo cha maisha gerezani kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16.

# TANROADS yatoa sababu uharibifu miundombinu

**Na Maulid Mmbaga**

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) umesema baadhi ya barabara kuharibika muda mfupi baada ya ujenzi, hakuna maana kwamba makandarasi hawakuzingatia viwango vya ubora wakati wa ujenzi, bali ni athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam wakati wa mkutano uliowakutanisha TANROADS, wahariri na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Mipango ya Miundombinu wa wakala huo, Ephatar Mlavi, alisema dunia imekumbwa na hali ya sintofahamu kutokana na matukio yasiyo ya kawaida ambayo hayakuwahi kuonekana siku za nyuma.

Mlavi ambaye alizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TANROADS, alisema hivi karibuni kumekuwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, hata wao wanajua kuna tatizo hilo na wanaendelea kutafuta njia za kukabiliana na changamoto hiyo.

"Tunajua kweli kuna mabadiliko ya tabianchi na wataalamu wengi kwetu sisi tunakuna vichwa ili kuona ni jinsi gani tunaweza tukajenga miundombinu yetu ili iweze kuwa na uwezo wa kuhimili mabadiliko hayo.

"Mabadiliko hayo si kitu ambacho tulikuwa tunategemea, kwa hiyo unakuta miundombinu imejengwa kwa usanifu na viwango vilevile vilivyokuwa vinatumika siku zote, lakini safari hii unakuta inajengwa na hesabu zilezile na mwisho wa siku inakuja kukumbwa na hali ambayo si ya kawaida," alisema Mlavi.

Alisema dunia hivi sasa inashuhudia ongezeko kubwa la mvua, baridi na joto kupita kiasi na kwamba hali hiyo ambayo aliwa ilikuwa ya kawaida, sasa imekuwa tofauti.

Kwa kuzingatia kuna changamoto hiyo, wakala utaendelea kushirikiana na wadau wengine "pamoja na kujiongeza" ili kuhakikisha unakuwa na miundombinu inayoweza kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Tutaongeza pia weledi kwa makandarasi wa ndani ili kukuza ufanisi," alisema.

Alieleza kuwa serikali imetoa dola milioni 325 (Sh. bilioni 886.5) kwa ajili ya kukarabati miundombinu iliyoharibiwa na mvua ya El-Nino na kimbunga Hidaya.

Akizungumzia ujenzi wa daraja katika eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam, Mlavi alisema tayari limeshasanifiwa na mkataba wake wa ujenzi utatiwa saini hivi karibu.

**MAFANIKIO**

Mlavi pia alisema miradi 38 ya ujenzi wa miundombinu ya barabara imekamilika katika mikoa 17, kati ya miradi 1,067 iliyoingiwa mikataba kuanzia mwaka 2019 hadi 2023, ikigharimu Sh. bilioni 411.

Alisema kuwa jumla ya Km 15,343.88 ziko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Kati yake, Km 1,198.50 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami, Km 2,031.11 ziko kwenye hatua za ujenzi, Km 2,052.94 na madaraja mawili zimefanyiwa upembuzi yakinifu.

Alitaja madaraja ambayo tayari yameshajengwa kuwa ni Gerezani (Dar es Salaam), Tanzanite (Dar es Salaam), Wami (Pwani), Kitengule (Kagera), Kiyegeya (Morogoro), Ruaha (Morogoro), Ruhuhu (Ruvuma), Mpwapwa (Dodoma) na Msingi (Singida).

Yanayojengwa ni Pangani (Tanga), John Magufuli (Mwanza), Lower Mpiji (Dar es Salaam), Mbambe (Pwani) na Simiyu (Mwanza).

Yanayotarajiwa kujengwa ni Godegode, Mtera (Dodoma), Ugala (Katavi), Kamshango, Kyabakoba, Kalebe (Kagera), Bujonde, Bulome, Ipyana (Mbeya), Chakwale, Nguyami, Mkundi, Mjonga, Doma, Mkondoa (Morogoro), Lower Malagarasi (Kigoma), Sanga (Songwe), Kilambo (Mtwara) na Chemchem (Singida).

# Mramba akaribisha Uingereza uwekezaji wa nishati jadidifu

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, amezikaribisha kampuni kutoka Uingereza kuwekeza kwenye sekta ya nishati hasa eneo la nishati jadidifu.

Amesema uwekezaji huo una azma ya kutimiza lengo la serikali la kuingiza umeme mwingi kwenye gridi ya taifa unaotokana na nishati hiyo.

Mramba alisema hayo jana jijini Dodoma alipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini Tanzania ukiongozwa na Euan Davidson, Kiongozi wa Timu ya Ustawi Endelevu katika kikao kilicholenga kujadili maeneo ya ushirikiano.

Mhandisi Mramba aliueleza ujumbe huo kuhusu mahitaji ya uwekezaji kwenye miradi ya nishati jadidifu ikiwamo umeme jua kwa ajili ya matumizi ya majumbani hasa kwenye sehemu zilizo nje ya gridi na uwekezaji mkubwa wa umeme jua utakaoingia katika gridi ya taifa.

Alisema tayari uwekezaji kwenye nishati ya umeme jua umeanza kupitia mradi wa Kishapu-Shinyanga wa megawati 150 na uwekezaji mwingine utafanyika kwenye maeneo mengine nchini ikiwamo mkoa wa Dodoma wenye uwezo wa kuzalisha megawati 200.

Kuhusu uwekezaji katika umeme unaotokana na upepo, alisema maeneo tayari yameshatambuliwa ambayo yanaweza kuzalisha yakiwamo Dodoma, Singida, Mbeya, Makambako, Same, Mara na Arusha ambayo yanahitaji ushirikiano katika uwekezaji.

"Tanzania tumebarikiwa vyanzo vingi vya nishati jadidifu kwani pia tuna hazina kubwa ya jotoardhi katika maeneo takriban 52 ambayo yakiendelezwa yatazalisha umeme kuliko Kenya ambayo sasa inazalisha umeme wa jotoardhi takriban megawati 1000," alisema. Pia alieleza nia ya Tanzania kutumia nishati safi zaidi kuzalisha umeme ikiwamo nishati ya blue hydrogen inayotokana na gesi asilia na matumizi nishati ya kinyesi cha wanyama na mabaki ya mimea (biogas) hasa katika vijiji yenye mifugo mingi.

Kuhusu nishati safi ya kupikia, Mhandisi Mramba aliueleza ujumbe huo juhudi zinazochukuliwa na serikali kuhakikisha asilimia 80 ya wananchi wanatumia iliyo safi kupikia ifikapo mwaka 2034. Alisema mpango huo ni utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, ambao utekelezaji wake unashirikisha serikali na wadau mbalimbali ikiwamo sekta binafsi.

Mhandisi Mramba alisema katika usambazaji wa umeme vijijini, Tanzania imepiga hatua kubwa kwenye eneo hilo na asilimia 99 ya vijiji vimefikiwa na nishati hiyo huku akibainisha kuwa ifikapo Desemba, mwaka huu, kila kijiji kitakuwa kimefikiwa na huduma hiyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jamii nzima inawajibika suala la ulinzi wa mtoto

**MATUKIO** ya ukatili dhidi ya watoto katika jamii nchini, yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara jambo ambalo limekuwa likitoa taswira hasi na kuliweka kundi hilo katika mazingira magumu.

Awali, matukio hayo yalikithiri kwa watoto na watu wenye ualbino ambao baadhi walikuwa wakitekwa na kukatwa baadhi ya viungo vyao huku wengine wakiuawa. Sababu kubwa ambayo ilikuwa ikitajwa wakati matukio hayo yakitokea ilikuwa ushirikina. Baadhi ya watu walikuwa wakiaminishwa kuwa ili wafanikiwe hawana budi kupeleka kwa waganga wa jadi viungo vya watu wenye ualbino kama vile sehemu za siri, mikono na viganja.

Hivi sasa, matukio hayo yamevuka mipaka na watoto wote kwa jumla, bila kujali hali zao wala jinsi, wamekuwa katika hatari. Wako wanaouawa, kutekwa na hata kufanyiwa vitendo viovu kama vile kulawitiwa, kubakwa na kunajisiwa. Hatua hiyo imesababisha watoto hao kuathirika kisaikolojia pia kukatisha ndoto zao za kufikia kiwango fulani cha masomo na matamanio yao wakiwa watu wazima.

Watoto wa kike wanaopatiwa ujauzito wakiwa shule za msingi au sekondari, wamekuwa wanakatisha masomo, hivyo ndoto zao za kuwa viongozi au wanasiasa baada ya kumaliza masomo ngazi za juu kutoweka. Baadhi ya vitendo hivyo vimekuwa vikifanywa na walimu walioaminiwa kuwafundisha watoto hao ili kutimiza ndoto zao, ndugu katika familia na baadhi ya walimu wa madrasa.

Aidha vitendo hivyo vimekuwa vikiota mizizi kwa sababu pindi baadhi vinapotokea, wahusika hawafikishwi katika vyombo vya sheria badala yake familia husika zimekuwa zikimaliza kimyakimya.

Hata vinapofikia hatua ya kufikishwa katika vyombo vya sheria, baadhi ya watu wamekuwa wakishindwa kufika mahakamani kutoa ushahidi, hivyo kesi kufutwa.

Kiongozi mmoja wa dini aliwahi kusema hivi sasa binadamu wamekuwa zaidi ya hayawani (wanyama, wadudu na viumbe vitambaavyo) kutokana na matendo wanayofanya na viumbe. Kiongozi huyo alisema ni vigumu ng'ombe dume kumwingilia ndama au jogoo kukipanda kifaranga lakini hali imekuwa tofauti kwa mtu mzima kumwingilia mtoto mdogo ambaye hajapevuka. Huo ndio ukweli halisi kutokana na mambo yatendekayo katika jamii kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Kuenea kwa matendo hayo kumesababisha watoto kuwa katika mazingira magumu kwa sababu akiwa shuleni, mathalani, hayuko katika mikono salama. Hiyo ni kutokana na kuwapo baadhi ya walimu ambao wanawafanyia unyama watoto hao. Wakienda kwenye mafundisho ya dini pia hawako katika mikono salama. Hata wakiwa njiani hakuna uhakika wa ulinzi kwa ajili yao. Kwa mantiki hiyo, hofu kuhusu usalama wao imetamalaki.

Viongozi wa serikali, dini na wanaharakati wameibuka na kutoa maoni na kauli kutaka vitendo hivyo vikomeshwe. Baadhi ya watu hao wametamka hadharani kuwa wanaopatikana na hatia wahasiwe au wanyongwe kutokana na sheria zilizopo kuonekana kwamba hazikomeshi vitendo hivyo.


Wakati kauli na maoni hayo vikitolewa, lawama kubwa zimekuwa zikipelekwa kwa serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama kwamba haiwajibiki ipasavyo katika suala zima la ulinzi kwa watoto.

Pamoja na lawama hizo na matamko yanayotolewa na viongozi na wanasiasa, ni vyema jamii ikatambua kwamba suala la ulinzi wa mtoto ni mtambuka. Kila mtu katika jamii ana wajibu wa kushiriki katika ulinzi wa mtoto kulingana na nafasi yake.

Kuna msemo katika mapambano dhidi ya UKIMWI usemao 'It Begins With You' (inaanza na wewe), pia suala la ulinzi wa mtoto ni la kila mtu kuanzia ngazi ya familia, jamii na taifa kwa ujulma.

Kwa mantiki hiyo, hakuna haja ya kunyooshea mtu au kikundi kuwa kimeshindwa kuwajibika katika ulinzi wa mtoto dhidi ya hatari zinazonyemelea au zinazomkabili. Kila mwanajamii anapaswa kuwajibika ili kuwalinda watoto dhidi ya hatari zozote zile.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tunaojichubua kwa vipodozi, pia tujiandae kwa aina madhara haya...

Na Sabato Kasika

**MATUMIZI** ya vipodozi visivyo salama, yanatajwa kuwa na madhara mengi katika mwili wa binadamu. Kwa kuwa vina madhara, serikali imepiga marufuku kuingizwa nchini, ili kulinda wananchi wake.

Baadhi ya madhara yanayosababishwa na vipodozi vilivyopigwa marufuku, yanatajwa na wataalam wa afya kuwa ni kupata saratani ya ngozi, uvimbe katika ngozi na inakuwa nyembamba.

Madhara mengine yanatajwa kuwa ni ngozi kuwa nyembamba na kutokuwa imara na haivutiki sana na kwamba mtu anayejichubua anapopata ajali, inamwia vigumu kushonwa kwa kuwa ngozi inakatika.

Vilevile, madhara mengine ni kutokwa na mabaka na vipele vikubwa ambavyo sio rahisi kupona na kwamba hufanya mtu akose mvuto na raha, ugonjwa wa pumu kutokana na krimu au vidonge kuathiri mapafu na mfumo wa upumuaji.

Wataalam wa afya wanataja madhara mengine, kuwa ni kupata watoto wenye kasoro za kiafya, kwa kuwa baadhi ya madini na viambata vilivyopo kwenye ving'arisha ngozi huathiri mbegu na mfumo wa uzazi.

Aidha, kuna matatizo ya akili na kuharibika kwa ini, kutokana na kushindwa kukabili sumu ya dawa ambazo mtu anatumia, kuharibika mishipa ya fahamu na figo kutokana na kiwango kikubwa cha zebaki (mercury) kilichomo katika krimu, kupungua kwa uzito wa mifupa. Hali inayoongeza hatari ya kuvunjika mifupa hiyo.

Matumizi ya vipodozi visiyo salama pia yanatajwa kusababisha kuungua uso na kubaki na ngozi yenye makovu isiyovutia.

Inaelezwa kuwa baadhi ya madhara hayo huonekana mara moja na mengine hujitokeza kadri mtu anavyotumia ving´arisha ngozi na kadiri anavyozidi kuzeeka.

Nadhani kwa madhara hayo, ni vyema jamii kuepuka vipodozi ambavyo si salama badala ya kuendelea kuvutana na serikali kwa kuviingiza nchini kinyemela.

Pia, watumiaji wanapaswa kutambua kuwa serikali inazuia vipodozi visivyofaa kwa sababu inajua vina madhara, badala ya kuvitafuta mafichoni na kwenda kuvitumia.

Mtindo wa baadhi ya wanawake kujichubua kwa vipodozi, ulianza miaka ya 80, umezidi kushamiri na umaarufu na sasa hata baadhi ya wanaume nao wakijichubua, kutafuta kuwa waupe.

Wakati hayo yakifanyika, wataalam wa afya ya ngozi tayari walishatahadharisha kuhusu madhara yake, huku serikali nayo ikivipiga marufuku, lakini ajabu ni kwamba watu wanavisaka mafichoni.

Lakini, inaelezwa kuwa watu wengi wamekuwa wakijichubua kwa kuiga wasanii wa nje na kushindwa kutambua kuwa, wasanii hao hufanya hivyo kwa usimamizi wa madaktari bingwa wa ngozi na kwa dozi maalumu, ili wasipate madhara yoyote.

Inasikitisha kuona serikali ikipiga marufuku dawa hizo, lakini baadhi ya watu wakiziingiza kwa njia za panya kana kwamba wanaikomoa serikali, kumbe wanajiua wenyewe kwa kutojua.

Kujichubua ngozi kunaweza kuwa ni janga la kimyakimya la kiafya, hivyo ingekuwa ni vyema kutafakari na kuchukua hatua ya kuachana na vipodozi visivyofaa, badala ya kuendelea kuving'ang'ania.

Hiyo inatokana na maelezo ya wataalam wa afya kuwa kuna madhara ya vipodozi yanaweza kujitokeza mara moja baada ya kuvitumia na mengine huonekana miaka ya uzeeni.

Ni muhimu kukumbuka kuwa, bidhaa za kung'arisha ngozi huwa na viambato hatari vinavyoweza kuwa na athari mbaya, na kutishia maisha vinapotumiwa kwa muda mrefu bila ushauri wa wataalam wa afya.

Kwa kuwa serikali ilishavitaja, ni vema jamii ikachukua hatua sahihi kwa ajili ya usalama wa afya ya ngozi na mwili mzima kwa ujumla, kwani vinginevyo ni kujitafutia hatari zaidi.

HABARI KITAIFA

# ‘Wafugaji chanzo migongano binadamu, wanyamapori’

**Na Jenifer Gilla**

WAKAZI wa Kijiji cha Mtelawamwahi, Kata ya Ligela, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, wameiomba serikali kudhibiti wafugaji wanaolisha mifugo ndani ya hifadhi kutokana na kusababisha ongezeko la migongano kati ya binadamu na wanyamapori.

Walisema tangu wafugaji hao walipoingia katika kijiji hicho na kulisha mifugo yao katika hifadhi migongano baina yao na wanyamapori imeongezeka kwa sababu idadi kubwa ya tembo wameondoka kwenye makazi yao na kuhamia kijijini hapo wakiikimbia mifugo hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari wanachama wa Chama cha Waandishi wa habari za mazingira Tanzania (JET) wakazi hao walisema hali hiyo inasababisha uharibifu mkubwa wa mazao yao kwa kuwa idadi kubwa ya tembo wanavamia mashamba tofauti na awali.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Rajabu Athumani, alisema wafugaji wanavyoongezeka ndivyo uharibifu wa mashamba unavyoongezeka na kutoa mfano mwaka jana walipokea kesi za malalamiko ya kuvamiwa mashamba kutoka kwa wakulima wanane, lakini mwaka huu zimefikia 14.

Alisema serikali ya kijiji kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi likiwamo Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), wanatoa elimu kwa wanakijiji namna ya kupunguza migongano hiyo kama vile kutofanya shughuli za kibinadamu karibu na hifadhi.

Alisema shirika la GIZ pia linawasaidia kuwapa elimu ya kutengeneza dawa zenye harufu kali kwa ajili ya kuzuia tembo kuingia kwenye mashamba yao hali iliyopunguza uharibifu kwa kiasi kikubwa. Alisema kama wafugaji wataendelea kulisha mifugo katika hifadhi, tembo wataendelea kuvamia mashamba na kwamba kunahitajika hatua za haraka za kuwaondoa watu hao.

“Kama unavyojua tembo ni mnyama mwenye akili sana, ukimwekea dawa katika shamba hili, kesho anahamia shamba la upande mwingine, pia ana uwezo wa kubuni njia mpya za uharibifu kila siku, kwa hiyo tunaomba serikali itusaidie kuwaondoa hawa wafugaji,” alisema.

Mtendaji wa kijiji hicho, Joseph Haule alisema kabla ya wafugaji hao, uharibifu wa mashamba haukuwa mkubwa, tembo wakiharibu robo heka ya shamba, lakini sasa wamekuwa wengi na kuharibu heka tatu za mkulima mmoja.

Askari wa wanyamapori wa kijiji hicho (VGS), Musa Nchimbi, aliiomba serikali na GIZ kuwaongezea idadi ya askari kwa kuwa wapo wachache na tembo wanazidi kuongezeka.

Aliomba pia kuwasaidia vitendea kazi zikiwamo pikipiki, viatu, mabomu ya kisasa ya kufukuzia wanyama ili kuwarahishia kazi pamoja na kuwalipa posho ili kuwapa nguvu ya kutekeleza majukumu yao kwa kuwa kazi hiyo wanaifanya kwa kujitolea.

Mkulima wa mahindi, John Mhagama, alisema elimu zaidi inahitajika ili kuwahamisha wafugaji na wakulima wanofanya shughuli zao karibu na hifadhi na hawana sababu yoyote ya msingi inayowapeleka katika maeneo hayo.

Alisema kuwapo kwa watu hao katika hifadhi pia Kunachochea shughuli za ujangiri wa wanyama pori ambao wanatumia mwanya huo kutekeleza shughuli zao.

Alisema mwaka jana tembo walivamia shamba lake la mahindi na kuharibu heka mbili ikimwacha na umasikini mkubwa na kulazimika kutafuta pesa za kumwezesha kulima mwaka huu.

Mhifadhi wa Wanyamapori wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Issa Hassan Ndomondo, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi wanafanya juhudi kubwa kupunguza migongano kati ya binadamu na wanyamapori katika vijiji vilivyopakana na hifadhi katika wilaya hiyo. Alisema wanatoa elimu kwa wafugaji wa namna ya kujikinga na wanyama waharibifu, kuwapa dawa za kufukuza wanyama wao pamoja na kuongeza nguvu kazi ya VGS kwa kuwapa mafunzo na mbinu mpya za kukabiliana na wanyamapori waharibifu katika maeneo yao.

Migongano hiyo inachochewa na wananchi kutokuwa na uelewa wa namna ya kujikinga na wanyamapori waharibifu na utayari wa kuwakubali wanyama hao na kuishi nao kwa tahadhari.

Mtelawamwahi ni moja ya vijiji vilivyo karibu na mapitio ya wanyamapori ya Selous-Niassa yanayounganisha Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Hifadhi ya Niassa ya nchini Msumbiji.

# Makinda: Sokoine alipenda uaminifu, hakuwa mnafiki

**Na Beatrice Shayo**

ALIYEKUWA Spika wa Bunge, Anna Makinda, amesema enzi za uhai wa Waziri Mkuu mstaafu, Hayati Edward Sokoine, aliwafundisha ukweli na uaminifu hakupenda unafiki.

Hayati Sokoine alifariki dunia kwa ajali ya gari mkoani Morogoro, Aprili 12, 1984 akitokea Dodoma kuelekea Mkoa wa Dar es Salaam.

Makinda aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati wa uchambuzi wa kitabu cha Hayati Sokoine ambacho kinatarajiwa kuzinduliwa Septemba 30, mwaka huu na Rais Samia Suluhu Hassan.

Kitabu hicho kitakuwa kinaelezea maisha ya Hayati Sokoine na uongozi wake kilichoandaliwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Uongozi na Chuo Kikuu cha Sokoine.

“Alitufundisha uaminifu na ukweli, hakuwa mnafiki kama umefanya kazi vizuri anakusifia, tuache unafiki na kujipendekeza kazi zetu zitatubeba kikubwa tuwe na matendo mema katika utekelezaji wa majukumu yetu,” alisema Makinda.

Aidha, alisema Sokoine alifanya kazi kwa bidii na alikuwa mfuatiliaji wa shughuli zote za serikali alipendwa na wananchi mbalimbali wakiwamo wa hali ya chini.

Balozi Ali Mchumo aliyefanya kazi na Sokoine kipindi kifupi, alisema mwaka 1975 aliteuliwa kuwa Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu na walifanya kazi katika Baraza la Mawaziri.

“Alivyoteuliwa uwaziri mkuu, Sokoine alisema ukiteuliwa kushika nafasi yoyote ukiaminiwa na wewe jiamini, hii kauli hadi sasa sijaisahau,” alisema.

Alisema mwaka 1977 hadi 1979 alibadilishwa kutoka ofisi ya waziri mkuu na kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, akisema wakati huo ndio vita ya Kagera na walipewa maagizo kuhamasisha wakuu wa mkoa kuanzia Mkoa wa Morogoro hadi Kagera kujipanga na jambo hilo.

“Wakati huo Sokoine alikuwa mwenyekiti wa kamati ya mawaziri wa vita, ilikuwa kila siku tunakutana asubuhi, kuna siku alinipigia simu mimi na Jackson Makweta (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu) akitutaka twende Kagera,” alisema.

“Asubuhi tukaondoka na Makweta kwenda Kagera alitupa maelekezo tuanzie Morogoro, hadi Kagera kuhamasisha wakuu wa mikoa kuandaa askari wa jeshi la akiba (mgambo) kwa ajili ya vita.”

Mchumo anasema yeye na Makweta walitekeleza jukumu hilo na baada ya kurejea Sokoine alitaka ripoti ya kazi aliyowapa ambayo inaelezea na sio maneno maneno.




Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel Tanzania, Dinesh Balsingh akikabidhi zawadi kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna alipowatembelea na ujumbe wake, katika makao makuu ya Airtel, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



MAKALA MAALUM

# Ana miaka 13 tayari anaitwa mama

**Na Elizabeth Zaya,**
SHINYANGA



Mwandishi wa Nipashe, Elizabeth Zaya akizungumza na mtoto aliyefanyiwa ukatili huo.

Ni simulizi ya kuhuzunisha inayomhusu mtoto wa miaka 13 (jina linahifadhiwa), mkazi wa Kishapu, mkoani Shinyanga, akiwasimulia baadhi ya wadau wa Mtandao wa Kutokomeza Ndoa za Utotoni Tanzania (TECMN) waliofika kwenye kituo anakolelewa.

Katika umri wake wa miaka 13 tayari anaitwa mama baada ya kaka yake ambaye ni mtoto wa mama yake mkubwa, kumpa mimba.

Akiwa darasa la sita mwaka jana, mtoto huyo (aliyezalishwa), alifiwa na wazazi wake wote wawili kwa nyakati tofauti akianza baba na kufuatia mama yake.

Kutokana na vifo vya wazazi wake, maisha yalikuwa magumu, ikabidi achukuliwe na mama yake mkubwa akaishi naye na akachukuliwa uhamisho ili akaendelee na masomo yake.

Nyumbani kwa mama yake mkubwa, alikuwa anaishi pia kaka yake ambaye ni mtoto wa mama yake huyo, aliyekuwa na mke na watoto. Alipofika, akawa anaishi nao akijua ni ndugu zake.

Chumba chake cha kulala alilala na binti mwenzake.

Anasema baada ya kukaa siku kadhaa pale nyumbani kwa mama yake mkubwa, maisha hayakuwa mabaya sana awali, lakini baadaye binti aliyekuwa analala naye alisafiri na hapo ndipo maisha yake yalipoanza kuwa 'machungu'.

Kuanzia siku hiyo kaka yake alianza kuingia chumbani kwake na kumwingilia kimwili kwa nguvu huku akimdanganya kumpatia fedha Sh. 500, na kwa kuwa alikuwa hajaizoea sana familia hiyo, aliogopa kumwelezea mtu yeyote madhila aliyokuwa akipitia.

"Kaka aliendelea mara kwa mara kuja chumbani kwangu usiku na kunibaka, alisema nisipige kelele, anasema atanipa Sh. 500. Niliogopa kumwambia hata mama mkubwa, wala mtu yeyote kwa sababu nilikuwa zijawazoea sana.

"Lakini baadaye nilianza kuugua, mama mkubwa aliponipeleka hospitalini wakasema nina mimba na akaniuliza ni ya nani, nikamwambia kaka ndiye alikuwa ananibaka kwa nguvu chumbani kwangu."

Anasimulia kwamba baada ya kupatiwa taarifa hizo kaka yake (aliyempatia ujauzito) alikimbia na hajulikani aliko mpaka sasa.

Baada ya kujulikana kwamba mtoto huyo alifanyiwa ukatili huo na kaka yake nyumbani alikokuwa akiishi, Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga uliamua kumpeleka katika kituo kinachosaidia mabinti na watoto wanaokumbwa na madhila ya namna hiyo kinachojulikana kama Agape Knowledge Open School cha mkoa huo.

"Walivyoniambia nina mimba wakanileta hapa kituoni, ndipo nikaanza kulelewa hapa mpaka sasa nimejifungua mtoto ana miezi minne," anasimulia.

Anasema kwamba, haelewi namna ya kumlea mtoto wake, kwa hiyo mara nyingi amekuwa anasaidiwa na mabinti wengine wanaomzidi umri waliopo katika kituo hicho.

Mtu mwingine anayemsaidia kulea mtoto wake ni mama anayeishi kituoni huko kwa ajili ya kuwasimamia.

Mlezi Mkuu wa Kituo hicho cha Agape, John Miyola, anasema mtoto huyo alifika kituoni kwake mwezi Machi mwaka huu na wakamsaidia kutatua baadhi ya changamoto za kiafya zilizokuwa zinamkabili na akafanikiwa kujifungua mtoto salama.

"Huyu binti alifiwa na wazazi wake wote kwa nyakati tofauti na wa mwisho kufariki alikuwa mama yake, sasa mama yake mkubwa alimchukua kwenda kumlea akiwa darasa la sita.

"Mama mkubwa alikuwa na kijana wake ambaye ana mke na watoto, kwa hiyo akawa akilala usiku anakwenda kumwingilia kimwili kwa nguvu.

"Binti akienda kuchota maji, akitoka shuleni, anamtumia, usiku anamtumia. Sasa ilifika kipindi mtoto akaanza kuugua ikabidi wampeleke hospitalini, na walipofanya vipimo ikagundulika kwamba tayari alikuwa mjamzito.

Anasema baada ya taarifa zile, kila mtu alishikwa na mshangao na hivyo ikabidi wampigie simu ili wamhamishie kituoni kwake wakati huo taratibu nyingine za kisheria zikichukuliwa.

"Kwa hiyo ilikuwa ni mshangao mkubwa kwa kila mtu kwa sababu ya umri wenyewe wa mtoto aliyepewa ujauzito, sasa hivi ana miaka 13 kwa maana hiyo wakati anapata ujauzito alikuwa na miaka 12, na kibaya zaidi hata yule kaka yake mwenyewe aliyemsababishia madhila hayo alikimbia, baada ya hapo, hospitalini waliamua kwamba wamlete hapa kituoni," anasema Miyola.

Anasema mtoto huyo alikuwa na changamoto ya damu pungufu, hivyo ilibidi wapambane kumpatia vyakula vya kuongeza damu.

"Katika hali yake hiyo ya ujauzito alikuwa na damu saba tu, kwa hiyo ikabidi tuanze kupambana kumpatia vyakula vya kuongeza damu na tulifanya hivyo mpaka ikawa sawa.

"Tumeishi naye hapa kuanzia Machi mwaka huu mpaka miezi tisa akaenda kujifungua, alipata changamoto kidogo, lakini Mungu ni mwema madaktari walipambana akajifungua salama na mwanawe ana miezi minne sasa," anasema Miyola.

Miyola anasema changamoto nyingine iliyomtokea mtoto huyo ni kukosa maziwa ya kumnyonyesha mwanawe na kulazimika kununua dukani.

Miyola anakiri kwamba mtoto huyo hana uwezo hata wa kumlea mwanawe, anasaidiwa na timu ya wenzake walioko kituoni.

"Huyu mtoto ni mdogo sana, yeye mwenyewe bado alikuwa anahitaji kulelewa kama ilivyo watoto wengine, kwa hiyo si rahisi ajue kulea, kuna mabinti hapa ni wakubwa kidogo wanamsaidia na wana mama anayewasaidia, kwa ujumla kituo ndio kimechukua jukumu la kulea hicho kichanga, wote ni watoto kwa hiyo wote wanalelewa," anasema Miyola.

Anasema baada ya mtoto kujifungua, walimsaidia akaendelea na masomo na amehitimu darasa la saba mwaka huu, anasubiri matokeo.

Lilian Kimati ni Mratibu wa Mtandao wa Kutokomeza Ndoa za Utotoni Tanzania, unaounda zaidi ya mashirika 80 ikiwamo la Msichana Initiative, Binti Makini Foundation, Theatre Arts Feminist Group, Medea, Plan International na My Legacy, anawaomba wadau mbalimbali kujitokeza kumsaidia mahitaji mbalimbali katika ulezi wa mtoto wake.

Pia wawasaidie mabinti wengine wanaosaidiwa katika kituo hicho ambao wengi wao wako huko baada ya kukumbwa na madhila mbalimbali zikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

Mipawa Ngusa ni Kaimu Mtendaji wa Kata ya Chibe wilayani ya Shinyanga Manispaa, mkoani Shinyanga, kilipo kituo anapolelewa mtoto huyo, anasema wakati anapelekwa kituoni hapo walishirikishwa na alikuwa na hali ya tatizo la afya ya upungufu wa damu, hivyo wakashauri asidiwe.

"Ni kweli tulishuhudia huyu mtoto alipoletwa hapa na baada ya kumwangalia kiafya alikuwa na shida ya damu, lakini alisaidiwa ikakaa sawa mpaka alipojifungua.

"Ni mtoto ambaye anahitaji msaada, kama kuna mashirika ambayo yanaweza kumsaidia tunaomba wajitokeze, si tu kwa huyu mtoto, lakini kwa mabinti wote waliopo katika kituo hiki maana wengi wamekutwa na madhila," anasema Ngusa.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 130 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, ni kosa la jinai kwa mtu mwanamume kumnajisi mtoto na adhabu yake imetajwa katika kifungu cha 131 cha sheria hiyo kuwa ni kifungo cha miaka 30 gerezani.



# H'shauri Mkinga yaanza kutumia sheria ndogo za ushuru

**Na Oscar Assenga,** MKINGA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, imeanza kutumia sheria ndogo za ushuru na uhifadhi wa rasilimali za pwani na bahari, ambazo zitatumiwa na vijiji saba vinavyotishiwa na ongezeko la shughuli za kiuchumi kwenye mwambao wa bahari ya hindi.

Vijiji vitakavyobanwa na sheria hiyo ni Moa, Kwale, Mongavyeru, Bomasubutuni, Bomakichaka Miba, Zingibar na Mwaboza.

Jana, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Amani Kasinya alisema kazi kubwa ya kuandaa sheria hiyo ya ushuru na uhifadhi wa rasilimali za pwani na bahari, imefanywa na Shirika la Mwambao.

"Ni lazima tuwape maua yao kwa sababu ya ushirikiano wao wa kuwezesha kusimamia na kuwezesha mchakato huu mpaka kukamilika kwake. Kwa muda mrefu, tulikuwa tukitafuta namna ya kufanya ili shughuli za kiuchumi katika mwambao wa Wilaya ya Mkinga, ziweze kufanikiwa kwa ukubwa wake.

**"Ni lazima tuwape maua yao kwa sababu ya ushirikiano wao wa kuweza kusimamia na kuwezesha mchakato huu mpaka kukamilika kwake. Kwa muda mrefu, tulikuwa tukitafuta**

"Lakini wadau hao wa mazingira, wakaona waje washirikiane nasi, ikiwemo kuwaweka walengwa kwenye vikundi na kuwapatia elimu, ambayo itawajengea utaratibu mzuri ambao utakuwa chachu kwao." alisema.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Rashid Gembe, alisema kwamba sheria hizo zitawapa alama katika mitandao duniani, kwa sababu hata mashirika na wadau wa maendeleo wanakuwa na amani kuona sheria zipo na zitekelezwa; hatua ambayo itavutia wengi.

Mratibu wa Shirika la Mwambao, Ahmad Salim, aliishukuru halmashauri hiyo kwa ushirikiano walioupata, huku akiahidi kuendeleza kusaidiana na mwanasheria wa Halmashauri ya Mkinga, kutoa elimu kwa wananchi na vikundi vya uhifadhi wa rasilimali za pwani na bahari, ili kuwajengea uwezo kuhusu sheria hizo.



Katibu wa Jumuiya ya Wazazi CCM, wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Nachia Ali (wa tatu kulia), akisalimiana na Mwenyekiti wa CCM Kata ya Tongwe, Ally Mhina kabla ya kuanza mkutano na viongozi na wanachama wa CCM katika ziara ya Kamati tendaji ya jumuiya hiyo wilaya ya kuhamasisha wananchi kujitokeza katika uchaguzi wa Serikali za mitaa, vijiji na vitongoji na baadaye kushiriki kufanya usafi katika Zahanati ya Kata hiyo, jana. Kutoka (kulia) ni Wajumbe wa Kamati hiyo, Baturi Dasi, na Jumanne Omari na (wa nne kulia) ni Katibu wa Elimu, Malezi na Mazingira wa jumuiya hiyo wilaya ya Muheza, Timotheo Martine. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wakazi Ngorongoro waombwa kushiriki Uchaguzi S/mitaa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

OFISA Uchaguzi wa Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha, Tumaini Saoyo, amewasihi wakazi wa Tarafa ya Ngorongoro inayokaliwa na idadi kubwa ya wafugaji wa jamii ya wamasai na maeneo mengine, kujitokeza kujiandikisha na kushiriki kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na watumishi wa wilaya hiyo kwenye kikao kazi cha kueleza nia hiyo ya serikali.

Saoyo alisema uboreshaji wa taarifa za kitambulisho cha mpiga kura na kuandikisha wapiga kura wapya kwenye Daftari la Mpiga Kura litafanyika kati ya Oktoba 11 hadi 20 mwaka huu.

Kikao hicho kiliitishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ngorongoro, Murtallah Mbillu.

Alisema lengo la kuchukua hatua hiyo ni kuhakikisha kuwa maeneo hayo yanapata uwakilishi mzuri wa kiutawala pamoja na huduma za kijamii na kiuchumi zinazowiana na mahitaji ya wananchi wake.

Katika uchaguzi huo, vyama 18 kati ya 19 vyenye usajili wa kudumu nchini vilihudhuria tukio hilo la kutangazwa tarehe ya uchaguzi huo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) hakikupeleka mwakilishi.

Septemba 16 mwaka huu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ilitangaza uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kurejesha takwa la kikatiba kwa wakazi wa Ngorongoro, mkoani Arusha na maeneo mengine nchini, kushiriki upigaji kura kwenye maeneo ya kiutawala ya vijiji 12,333 vilivyokuwa vimefutwa.

Hatua ya urejeshaji wa vijiji hivyo inatokana na maeneo yaliyokuwa yamefutwa awali kwa mujibu wa Tangazo la Serikali, Namba 673 na 674, ambayo yalihusisha, pia Tarafa ya Ngorongoro inayokaliwa na idadi kubwa ya wafugaji wa jamii ya kimasai.

Serikali ilivirejeshea huduma vijiji 65 na vitongoji 242 vya wilaya hiyo kama takwa la kikatiba la kushiriki upigaji kura kwenye maeneo ya kiutawala ya vijiji vilivyokuwa vimefutwa.

# Maofisa ofisi ya AG wapigwa msasa uandaaji bajeti

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

OFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeanza kuwapiga msasa maofisa wake ili wapate ubobezi katika uandaaji wa mpango na bajeti na utaalam wa kuhusianisha mfumo wa mapato na matumizi wa muda wa kati (MTEF) na mpango mkakati.

Maofisa hao wa bajeti wanatoka divisheni, vitengo na ofisi za mikoa za Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Akizungumza jana jijini hapa, wakati akifungua mafunzo ya siku tatu yaliyoanza Septemba 25 hadi Septemba 27, Mkurugenzi wa Divisheni ya Mipango, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Buji Bampebuye, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea na kuwaongezea uwezo watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika masuala yanayohusu mipango na bajeti.

Mafunzo hayo yameandaliwa na kuendeshwa na Divisheni ya Mipango Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano na wataalamu kutoka Wizara ya Fedha.

Aidha, Bampebuye alisema maofisa hao watapata kufahamu namna ya kupangilia na kuandaa bajeti, kuandaa na kutekeleza mpango kazi na mtiririko wa fedha, kuandaa mfumo wa mapato na matumizi wa muda wa kati (MTEF) pamoja na ufutailiaji na udhibiti wa bajeti.

Alisema: "Mafunzo haya kwa mwaka huu tumeona tuyafanye kwa kuwahusisha wataalamu kutoka Wizara ya Fedha ili waje kutuongezea ujuzi zaidi, nawaomba muwe huru kuuliza maswali kuhusu suala lolote linalohusu bajeti".

Shedrack Ndaile, ambaye ni mtaalamu wa masuala ya bajeti kutoka Wizara ya Fedha, alisema moja ya vitu wanavyopaswa kuvizingatia kwa sasa ni namna ya uundaaji wa bajeti, uidhinishaji wa bajeti na utekelezaji wa bajeti.

Aliyataja mambo mengin ni ufuatiliaji na udhibiti wa bajeti pamoja na mfumo wa MTEF, ambapo aliwaelekeza kwa kina mchakato wa uandaaji wa bajeti unavyofanywa na serikali na baadaye katika ngazi ya taasisi.

Wakili wa serikali anayesimamia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mkoani Arusha, Veritas Mlay, aliishukuru divisheni ya mipango, kwa kuandaa mafunzo maalumu ya bajeti akisema yatawasaidia maofisa bajeti kuongeza uelewa kwenye masuala mbalimbali yanayohusu mipango na bajeti.







Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha akizungumza wakati akifungua maadhimisho ya 11 ya Wiki ya Viziwi Duniani, juzi, ambayo kitaifa yanatarajiwa kufanyika mkoani humo kesho. Macha, aliwataka watu wenye ulemavu mbalimbali wajitokeze kugombea nafasi za uongozi kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa na kupiga kura kuchagua viongozi makini watakao waletea maendeleo na kutatua shida zao. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Bil.3/- yarudisha tabasamu kwa wananchi 5,000 Rusumo

**Na Judith Julius,** NGARA

ZAIDI ya wananchi 5,000 kutoka Kata ya Rusumo wilayani Ngara mkoani Kagera wameanza kunufaika na huduma ya maji safi na salama, baada ya mradi wa maji wa Rusumo uliogharimu Sh. bilioni tatu kuanza kutoa huduma.

Akizindua mradi huo juzi uliotekelezwa na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) juzi, Kiongozi wa Mwenge wa Uhuru, Godfrey Mzava aliutaka RUWASA kuusimamia ipasavyo mradi huo ili uendelee kuwahudumia wananchi pamoja na wananchi kutunza miundombinu yake.

Akisoma taarifa ya mradi huo, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Ngara, Saimon Ndyamkama alisema mradi huo ulianza kutekelezwa Oktoba 2020 na umekamilika na kuanza kutoa huduma Januari, 2024.

Alisema mradi huo umetekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) na umewapunguzia wananchi zaidi ya 5000 adha ya kufuata maji umbali mrefu ikiwa ni sambamba na kupunguza magonjwa yanayosababishwa na matumizi ya maji machafu.

**Kadhalika, alisema Serikali ya Zanzibar imeanza uchunguzi wa miradi ya maendeleo 70 na kubaini kuwepo kwa kasoro za kiutendaji zinazohusu ubadhirifu wa mali ya umma.**

Mbunge wa Jimbo la Ngara, Ndaisaba Ruhoro alisema wananchi wa kata hiyo wameishi bila kupata huduma ya maji safi na salama tangu uhuru, hivyo kuishukuru serikali kwa kutekeleza mradi huo na kuufanya ukomo wa mateso kwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Kahabi, aliahidi kutekeleza kwa wakati maagizo yaliyotolewa na kiongozi wa mbio za mwenge kwani kufanya hivyo jukumu lake.

Kabla ya Mwenge wa Uhuru kutamatisha ziara yake wilayani Ngara ulikagua miradi yenye thamani ya zaidi ya Sh.bilioni 5.1, huku ukiwa na kaulimbiu isemayo "Tunza mazingira na shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ujenzi wa taifa endelevu'.

# RC aagiza maofisa habari kusomea lugha ya alama

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha ameziagiza halmashauri mkoani hapa kuhakikisha zinatenga fedha kila mwaka kuwapeleka maofisa habari, mawasiliano na uhusiano kwa umma ili kujifunza lugha za alama.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akifungua maadhimisho ya 11 ya wiki ya viziwi duniani yanayotarajiwa kufanyika kitaifa mkoani hapa katika viwanja vya Sabasaba Manispaa ya Shinyanga.

Alisema viziwi hawana tofauti na watu wengine, bali hutofautishwa na lugha ya mawasiliano tu, hivyo kutaja hatua hiyo kuwa msaada katika kuendelea kukuza lugha ya alama na kusaidia utolewaji wa huduma muhimu kwa kundi hilo. Kadhalika, alizitaka taasisi zote za serikali pamoja na binafsi, kuhakikisha wanakuwa na wakalimani wa lugha ya alama, ili kusaidia kutoa huduma stahiki kwa watu viziwi wanapofika kwenye taasisi hizo.

Kuhusu ajira kwa wenye ulemavu, Macha alizitaka taasisi zote za serikali na binafsi kuzingatia zinatekeleza takwa la kisheria linalohusu asilimia tatu ya ajira iwe kwa wenye ulemavu.

"Niwasihi sasa wazazi msiwafiche ndani watoto wenye ulemavu bali wapatie elimu sawa na watoto wengine, kwani serikali imeboresha mazingira na miondombinu ni rafiki ya watoto hao kusoma," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), Selina Mremba, alisema lugha ya alama ndiyo chombo cha mawasiliano kwa viziwi, kusisitiza suala la kuwepo kwa wakalimani wa lugha hiyo kwenye taasisi zote za serikali na binafsi. Aidha, aliwata kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wajitokeze kuwania nafasi za uongozi, pamoja na kushiriki kupiga kura ili kuchagua viongozi watakaowaletea maendeleo na kutatua shida zao.

Mwakilishi Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) Ghati Horombe, alisema ili taifa lifikie maendeleo endelevu, lazima ujumuishwaji wa makundi yote ufanyike bila ubaguzi yashirikishwe.

Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi wilayani Kahama, Zawadi Masoud, akisoma risala aliomba kuwepo na wakalimani wa lugha ya alama kwenye taasisi za serikali na binafsi, ikiwamo polisi, mahakama na hospitali, ili kusaidia upatikanaji wa mawasiliano pale wanapofika kupata huduma.

Masound aliiomba serikali kutenga bajeti katika halmashauri kusaidia viziwi kushiriki kwenye maadhimisho ya kitaifa, pamoja na kushirikishwa kwenye vikao mbalimbali vya maamuzi.

Kilele cha maadhimisho ya kumi na moja ya viziwi dunia, yatafanyika Septemba 28 mwaka huu, kitaifa yatafanyikia mkoani Shinyanga yakiwa na kauli mbiu isemayo "Ungana kutetea haki za lugha ya alama".

# Mkemia aonya matumizi holela ya zebaki

**Na Mohab Domonick,** KAHAMA

MENEJA wa maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Ziwa, John Wanjara amesema kemikali ya zebaki ni hatari kwa afya ya binadamu, mifugo na mazingira.

Hivyo, amewaonya wachimbaji wa madini juu ya matumizi holela ya kemikali hiyo.

Wanjara alitoa tahadhari hiyo juzi katika semina ya watumiaji wa zebaki katika mgodi wa Mwime uliopo katika Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga na kueleza kuwa serikali kwa sasa imesitisha matumizi yake kwa wachimbaji.

Alisema kuwa uchafuzi wa mazingira unasababishwa na matukio ya asili na matumizi ya binadamu na kuongeza kuwa wachimbaji wanapo chenjua dhahabu mabaki yanayosalia yanaharibu mazingira.

Aidha alisema kuwa miongoni mwa njia za kujikinga na madhara ya kemikali hiyo ni pamoja na kuitunza kwa usahihi kwa kuijengiea eneo lake katika mialo ya uchenjuaji.

Pia, kutokuenda nayo nyumbani na kutumia vifaa sahihihi katika kujikinga wakati wa kazi zao.

Baadhi ya wachimbaji wa madini katika mgodi huo akiwemo, Njile Nkuba walisema licha ya wao kujikinga bado kuna mifugo kama mbuzi, ng'ombe na kuku inayozunguka kwenye maeneo ya uchenjuaji.

Alisema hatua hiyo ni hatari pindi mtu akichinja mifugo hiyo kwa ajili ya kitoweo.

Akizungumza katika semina hiyo, ofisa kutoka katika ofisi ya Ofisa Madini Mkazi Wilaya ya Kahama, Wiliamu Msukiula aliwataka wamiliki wa mialo kuwa waaminifu na kutoa ushirikiano wanapokuwa wanahama au kusimamia uzalishaji katika maeneo yao.

Alisema mialo mingi katika mgodi wa Mwime haifahamiki dhahabu zake zinauzwa katika maeneo gani.

Alisema wamekuwa mstari wa mbele katika kutoa elimu juu ya madhara ya utoroshaji wa madini katika maeneo mbalimbali ya uchimbaji, huku akiwataka wachimbaji kuwa waaminifu katika kazi yao.



Ukurasa 12

**Matumaini, kicheko umeme kuifanya Kigoma kitovu cha uchumi na biashara**




Ukurasa 13


Wasiojulikana sasa wanavamia sanamu ya Nyerere kuibomoa!


# BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 27, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ukurasa 14

**Pigo Uviko 19 China lilivyowafunza kinamama ubahili na bajeti kipato**

BIASHARA

# SAMIA RASMI AIFANYA MBAMBABAY KARIAKOO

- Azindua Km. 66 ushoroba kuunganisha Mtwara
- Bil. 80/- zawekezwa bandarini, Malawi kufikike
- Aagiza kituo kupatikana vyote vilivyoko Dar

**Na Mwandishi Wetu**

NI faraja kwa wakazi wilayani Mbamba Bay mkoani Ruvuma kukombolewa kwa mawasiliano, historia yenye unasaba hata mkoa husika, wilaya hiyo haikufikika kirahisi kimawasiliano.

Zama hizo walitumia mbadala kupitia Ziwa Nyasa kutoka Bandari ya Itungi Kyela, pindi wana safari za mbali kwenda mikoa kama Dar es Salaam na Iringa na kwenda Songea, safari ilikuwa ngumu sana.

Simulizi hiyo iko hata kabla ya mwaka 2006, ilikuwa katika ugumu hakupitiki hadi kulipojengwa Barabara kati ya Masasi kupitia Tunduru mkoani Mtwara na nyingine kutoka Tunduru , hadi kufika Namtumbo, ikiwa ni juhudi zake Rais Dk. Jakaya Kikwete katika awamu yake ya uongozi.

Hata ikirejewa nyuma zama miaka ya 1980 ndio kulijengwa barabara kukwepa mlima mkali uliounganisha mkoa huo na Njombe, wakati huo ulikuwa sehemu ya mkoa wa Iringa.

Hiyo maana yake mabadiliko ikaufungua mkoa wa Ruvuma kufikika kirahisi, mathalan kuna mabasi sasa yanayoenda Songea kutoka Dar es Salaam, kupitia Masasi na mengine yanapitia Njombe.

Mikakati hiyo inapounganishwa na maboresho ya mkoa kufunguka kupitia kutanuliwa Uwanja wa Ndege na mageuzi yanayoendelea ndani a Ziwa Nyasa, inayounganisha mkoa Mbeya kupitia Bandari Itungi, pia nchi jirani za Msumbiji na Malawi.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiweka jiwe la Msingi la Ujenzi wa Bandari ya Mbamba Bay, katika Ziwa Nyasa mkoani Ruvuma juzi. **PICHA: MTANDAO.**

**UGENI WA SAMIA**

Ugeni wa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan juzi wilayani Mbamba Bay yakatokea mambo mawili. Moja, Rais akazindua mradi wa ujenzi wa bandari ukigharimu shilingi bilioni 80.

Pili, ni uzinduzi wa Barabara ya Mbinga - Mbamba Bay yenye urefu kilometa 66 imekamilika kiwango cha lami, mjenzi kampuni kutoka China na Mshauri Mjenzi, kutoka Australia.

Hapo ikatumika shilingi bilioni 122.76 za ujenzi na shilingi milioni 637.4 zilizotumika kulipa fidia kwa wananchi walioathirika na ujenzi.

Mradi huo wa barabara ya Mbinga - Mbamba Bay, ni sehemu ya barabara kuu ya ushoroba wa Mtwara yenye urefu wa kilometa 826, inayoanzia Mtwara mpaka Mbamba Bay na Rais Dk. Samia anasema, inauganisha Bandari za Mtwara na Mbamba Bay.

Pia, ndio eneo inayounganisha mkoa wa Ruvuma na wa Mtwara na mkoa wa Mbeya na nchi jirani Malawi kupitia Ziwa Nyasa, huku ikifafanuliwa juzi, inaunganisha bandari za Mtwara na Mbamba Bay.

Uzinduzi wa jana unatajwa kuwa sehemu ya mafanikio ambayo aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Malawi, Humphrey Polepole mwezi Septemba mwaka 2022, alifanya ziara kutazama fursa katika ushoroba wa Mtwara hadi Bandari Ndumbi.

Akafafanua wakati huo kuwa, serikali inatarajia kuanzisha Kanda Maalum ya Kiuchumi huko Mbamba Bay Ziwa Nyasa wilayani Nyasa mkoani Ruvuma, kuhakikisha bidhaa zote zinazopatikana Kariakoo jijini Dar es Salaam zinapatikana Nyasa.

Wakati anamwaapisha Waziri wa Biashara na Viwanda Julai mwaka huu, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akamuelekeza kuwajibikia ufanisi wa Kariakoo kibiashara, kwa maana ni kituo cha kimataifa cha biashara, huku nchi ya Malawi ni sehemu ya wateja wakuu wanaopatikana hapo.

Balozi Polepole akizungumza wakati huo baada ya kukagua Bandari kongwe ya Mbamaba Bay na bandari mpya ya Ndumbi, ambayo serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 12 kujenga, akatoa rai wadau kuwa tayari kutumia fursa zinazopatikana katika ushoroba wa Mtwara.

"Ushoroba huu ni wa barabara inayotoka Bandari ya Mtwara na inakuja kwa kilometa 822 mpaka bandari ya Mbamba Bay, ushoroba huu katika Kusini mwa Afrika, ndiyo ushoroba bora zaidi na mfupi kuliko shoroba nyingine zote," akasema.

**INAENDELEA UK.14**

BIASHARA

# Matumaini, kicheko umeme kuifanya Kigoma kitovu cha uchumi na biashara

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa Kigoma**



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kushoto) akiweka jiwe la msingi katika mradi wa Kufua Umeme Mto Malagarasi MW 49.5 mkoani Kigoma. Kulia ni Mkuu wa Mkoa huo, Thobias Andengenye. **PICHA; MAKTABA**

SEPTEMBA 19, 2024 ilikuwa siku ya kihistoria katika mkoa wa Kigoma.

Ilikuwa siku ya kufungua ukurasa mpya kwa sura ya mkoa huo ambao kwa miaka mingi umekuwa nyuma kiuchumi licha ya kuwa na fursa mbalimbali ambazo zingeufanya kuwa juu kimaendeleo.

Miongoni mwa sababu zilizofanya mkoa huo kuwa katika hali hiyo ni miundombinu ya usafiri hasa barabara na kukosekana kwa umeme wa uhakika ambao ungechochea uwapo wa viwanda vya kuchakata bidhaaa mbalimbali na kutoa ajira za moja kwa moja na sizizo za moja kwa moja.

Katika suala la usafiri Kigoma ilikuwa ikitegemea zaidi reli ya kati ambayo inaishia hapo kutoka Dar es Salaam ndiyo maana ikapewa jina la 'Mwisho wa Reli'. Hata hivyo, usafiri huo kwa miaka kadhaa haukuwa wa uhakika kutokana na kuyumba kiutendaji kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Pia usafiri wa ndege umekuwa tegemeo kwa wananchi wa mkoa huo lakini nao umekuwa si wa uhakika na si wananchi wote wana uwezo wa kutumia aina hiyo. Sababu kubwa ni hali ya kiuchumi kwa kuwa wenye uwezo wa kumudu gharama za usafiri huo ni wachache.

Kuwapo kwa changamoto ya aina hizo za usafiri, kuliwalazimu watu wanaokwenda na kutoka Kigoma kwenda mikoa mbalimbali kutumia barabara ambazo nazo hazikuwa za lami. Waliotumia usafiri huo walipata shida njiani kutokana na ubovu wa barabara, mabasi yaliyokuwa yakienda na kutoka huko yalikuwa mabovu kiasi cha kuwafanya wasafiri kutumia hata siku tatu njiani.

"Enzi zile kabla ya barabara za lami, haikuwa shida ukiwa Mwanza au Dar es Salaam kumtambua mtu aliyekuwa akitoka Kigoma. Ulikuwa unamtambua kwa vumbi tu lakini sasa ni historia," alisema Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, wakati wa uwekaji mawe ya msingi ya mradi wa kuzalisha umeme katika mto maporomoko ya Malagarasi na kituo cha kupokea, kupoza na kusambaza umeme wa gridi ya taifa cha Kidahwe.

Kutokana na changamoto hizo, serikali ilifanya jitihada za kuifungua Kigoma kwa aina zote za usafiri ili kuchochea kasi ya maendeleo na kuwa kitovu cha maendeleo.

Mkoa sasa umefunguliwa kwa barabara za lami na sasa kuna usafiri wa uhakika kutoka kona zote kuingia Kigoma. Waliokuwa wakisafiri kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma kupitia Kasulu, umbali wa kilometa 1,298 wanatumia wastani wa saa 18. Kwa wale wa kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma kupitia Tabora, wanatumia saa 19 hadi 20 kutokana na baadhi ya maeneo kutokukamilika kwa ujenzi wa kiwango cha lami.

> **"Kwa jumla, wanufaika wakubwa wa umeme ni TAMISEMI kwa sababu ndio wasimamizi wa sekta za elimu na afya. Ukienda katika afya, umeme unahitajika kwa sababu kuna mashine za maabara na vipimo ambazo zinahitaji umeme.**



Zaynab Katimba

Jitihada zaidi zinaendelea kuifungua Kigoma kwa reli ya kisasa (SGR) ambayo kwa sasa ujenzi umekamilika kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na kazi inaendelea Makutopora (Dodoma) hadi Tabora na hatimaye Kigoma. Usafiri huo utakapoanza utaifungua zaidi Kigoma na kupanua fursa za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

### HATIMAYE UMEME

"Sasa umeme wa uhakika wa gridi ya taifa unaanza kuingia Kigoma. Ile historia ya kuwa moja ya mikoa iliyo nyuma kiuchumi inafutika. Tulianza na barabara, tunakuja na umeme hatimaye treni ya kisasa (SGR). Nuru inawaka Kigoma," alisema Dk. Biteko.

Kama ilivyokuwa kwa mikoa ya pembezoni kama Kagera, Rukwa na Katavi, Kigoma ilikuwa ikitumia majenerata kuzalisha umeme hali ambayo ililisababishia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) gharama kubwa za uendeshaji na kuliingizia hasara.

Kwa mujibu wa Dk. Biteko, kwa mwaka TANESCO imekuwa inatumia Sh. bilioni 35 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta mazito ambayo hutumika kwa ajili ya kuzalisha umeme.

"Pamoja na kutumia fedha hizo, ukiangalia kiasi kinachopatikana kwa ajili ya kuuza umeme ni Sh. Bilioni 16, hivyo shirika linapata hasara ya Sh. bilioni 19. Kwa hiyo ulikuwa mzigo mkubwa na sasa tutauondoa," alisema.

Licha ya matarajio ya kupata umeme wa gridi ya taifa megawati 49.5 baada ya kukamilika kwa mradi huo, Kigoma pia itaanza kupata umeme wa gridi ya taifa katika njia zingine hali itakayowezesha kuufungua zaidi mkoa kiuchumi.

Kwa hatua hiyo, Kigoma iliyokuwa moja ya mikoa ya pembezoni sasa itageuka kuwa kitovu cha nishati na itaufanya mkoa kupiga hatua za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

"Kigoma sasa itafunguka kimaendeleo kwa sababu ya umeme wa gridi ya taifa. Baada ya kufunguka kwa miundombinu ya usafiri, sasa ni zamu ya kufunguka kwa umeme na hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kasi ya maendeleo katika nyanja mbalimbali," alisema.

Katika kufanikisha azma ya Kigoma kuwa kitovu cha nishati, serikali imetoa Sh. trilioni 1.2 ambazo pamoja na ujenzi wa mradi wa Malagarasi, zitatumika kupokea, kupoza na kusafirisha umeme kutoka Nyakanazi kilovoti 620, ujenzi wa njia ya Tabora - Uvinza hadi Kigoma, Katavi hadi Uvinza kilovoti 220 kwa ajili ya treni ya SGR.

### KAULI YA TANESCO

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Boniface Nyamohanga, alisema

umeme wa gridi ya taifa utalipunguzia mzigo shirika wa uzalishaji na kuwa na umeme wa hakika ambao utachochea kasi ya ukuaji wa uchumi wa mkoa, maisha bora ya wananchi na pato la taifa.

"Umeme huu pia utasaidia kuboresha huduma za kijamii kama elimu na afya. Pia utatengeneza ajira za muda mfupi na mrefu. Zaidi ya wafanyakazi 700 wanatarajiwa kuajiriwa.

"Licha ya manufaa hayo, gharama za uzalishaji wa umeme zitapungua kwani tutaondoa majereta ambayo yalikuwa yakitumika kuzalisha umeme ambayo yalikuwa mzigo mkubwa kwa shirika.

"Kigoma ni moja ya mikoa ambayo ilikuwa haijaunganishwa na gridi ya taifa, hivyo kupata umeme kupitia mitambo ya uzalishaji inayotumia mafuta ambayo imekuwa ikiligharimu Shirika fedha nyingi kwa ajili ya uendeshaji na hasa mafuta ambayo miezi ya hivi karibuni bei zake duniani zimekuwa zikipanda.

"Kwa upande wa Kigoma mjini, umeme unazalishwa kwa kutumia mitambo ya mafuta iliyopo Kigoma (Megawati 8.75) na pia umeme wa jua unaozalishwa (kiwango cha juu Megawati 4.7) kutoka kwa kampuni binafsi NextGen Solar (SOLAWAZI)," alisema.

Kuhusu Kasulu na Kibondo, alisema umeme ulikuwa unazalishwa kwa kutumia mitambo ya mafuta iliyoko Kasulu (Megawati 3.75) na Kibondo (Megawati 2.5) huku akibainisha kwamba mitambo ya Kasulu pia ilikuwa inapeleka umeme katika wilaya ya Buhigwe.

Kwa mujibu wa Mhandisi huyo, gharama za uendeshaji kwa wastani kwa mwaka katika wilaya ya Kibondo zilikuwa Sh.bilioni 9.44, Kasulu (Sh.bilioni 12.94 na Kigoma mjini ni Sh. bilioni 35.78, hivyo kufanya jumla ya gharama kuwa Sh. 58.16 kwa mkoa mzima.

"Mapato ya mauzo ya umeme kwa mkoa wa Kigoma ni wastani wa Sh. bilioni 16.09 ambayo ni chini ya asilimia 30 ya gharama yote inayotumika kuzalishia umeme huo," alisema nak ubainisha kuwa kwa sasa kuna unafuu wa kupungua kwa mzigo huo wa gharama baada ya mkoa kuanza kupata umeme wa gridi ya taifa.

"Kwa sasa, maeneo ya Kasulu, Kibondo na Buhigwe yanapata umeme wa Gridi ya Taifa kupitia njia ya msongo wa kilovoti 33 kutoka Nyakanazi, hivyo kuwezesha shirika kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 22.38 kwa mwaka," alisema Nyamohanga.

Kuhusu mradi wa Malagarasi, Nyamohanga alisema ni Dola za Marekani Milioni 144.14 (takribani Sh. bilioni 389) ambazo serikali inagharamia Dola za Marekani milioni 4.14 na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inagharamia kiasi cha Dola za Marekani Milioni 140.

Kwa mujibu wa Nyamohanga, kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme wa uhakika katika mkoa wa Kigoma na mikoa jirani, hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuchochea maendeleo ya mkoa sambamba na kupunguza gharama za uendeshaji wa shirika kwa kuondoa majenereta.

### KUZIMWA MAJENERETA

Kutokana na jitihada hizo, Biteko aliagiza shirika kuzima majenereta yanayotumika kuzalisha umeme ifikapo mwishoni mwa mwaka huu huku wakati wa hafla hiyo kukiwa na mabango yenye ujumbe mbalimbali likiwamo lililosomeka: "Mradi ukikamilika tutazima majenereta na kuwasha umeme wa gridi ya taifa."

Bango lingine lilisomeka: "Kuunga Kigoma kwenye gridi ya taifa kutaimarisha hali ya upatikanaji wa umeme." Hali hiyo inaweka matumaini mapya ya mkoa wa Kigoma kupata umeme wa uhakika ambao utazaa neema tele za kimaendeleo katika sekta mbalimbali.

### KUFUNGUKA KIUCHUMI

"Umeme wa uhakika kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi." Hilo ni bango lingine ambalo linaonesha moja ya mafanikio yanayoweza kupatikana kutokana na uwapo wa umeme huku lingine likisema: "Kukamilika kwa mradi kutaifungua Kigoma kiuchumi."

Ujumbe huo unahanikizwa na kauli ya Mkuu wa Mkoa, Thobias Andengenye, kwamba hatua hiyo itaifungua Kigoma na kuwa kitovu cha Uchumi na biashara huku akisisitiza kuwa mradi huo utaondoa changamoto za kiuchumi zilizosababisha mkoa kurudi nyuma.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Zaynab Katimba, ambaye pia ni mzaliwa wa Kigoma, alisema katika hafla hiyo kuwa ujio wa umeme wa gridi ya taifa, unaifanya Kigoma kung'ara katika sekta mbalimbali zikiwamo za uchumi na kijamii.

"Kwa jumla, wanufaika wakubwa wa umeme ni TAMISEMI kwa sababu ndio wasimamizi wa sekta za elimu na afya. Ukienda katika afya, umeme unahitajika kwa sababu kuna mashine za maabara na vipimo ambazo zinahitaji umeme.

"Pia katika elimu, kuna maabara ambazo vifaa vyake vinahitaji umeme. Kwa kweli ujio huu wa umeme wa gridi ya taifa utainufaisha Kigoma katika sekta hizo. Lakini pia utachochea maendeleo ya viwanda na kuufanya mkoa wa Kigoma kuwa katika chati ya juu kimaendeleo," alisema Katimba.

Ni ukweli kwamba Kigoma ni mkoa wa kimkakati katika biashara kutokana na kupakana na nchi jirani za Burundi na Jamhuri yua Kidemkorasi ya Congo (DRC). Kwa hiyo uwapo wa miundombinu bora ya usafiri na umeme wa uhakika, utachochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa mkoa na pato la taifa kwa ujumla.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wasiojulikana sasa wanavamia sanamu ya Nyerere kuibomoa!






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

NIKO nyumbani sina hili wala lile, nawaza tu uhusiano wa mkono na kinywa changu utakuwaje leo, pia nikiwaza hivyo hivyo kwa niaba ya familia, mara anaingia jirani yangu Deo Alufonsi, ambaye huwa hana la kusema, liwe jungu au ubuyu.

Namwona ana kimuhemuhe cha kutaka kuniambia jambo lililomshitua na kumshangaza, simkatizi namkaribisha, namruhusu na kumwomba amwage ujugu alionao nami nifaidike.

Kwa lafudhi ya Kihaya, ananiambia kuna jambo limetokea Tabora na kuniuliza kama nalijua, hivyo namtaka amwage upupu hadharani nisipitwe pia na ubuyu wa siku.

"Mutani, Wanyamwezi wameharibu huko kwao, wameangusha sanamu la mutani wangu mwingine, Bhabha wa Taifwa letu, Mwalimu Nyerere,

wameondoka na shingo na kifwimbo chake, alichokuwa akitembea nacho!

In fwakti wamefwanya vya ajabhu.

"Yaani hawa Wanyamwezi wamekuwa na akili ya ngombe, kungangania sanamu kubwa kama lile na kuliangusha chini na kulibomowa na kuondoka na viungo vyake, kwa kweli wamefwanya vya kustaajabisha kweli!"

Namwelewa Deo na mimi nabaki kushangaa, kuwa nchi hii leo kuna mtu anaweza kubomoa sanamu la Mwalimu Nyerere kweli? Sanamu la Baba wa

Taifa, mtu mwenye mchango mkubwa wa uhuru wa nchi hii, aliyeacha alama isiyofutika.

Nikajiuliza inakuwaje sanamu la askari pale makutano ya Azikiwe na Samora liko imara na halichezewi na hata barabara ya mwendokasi inayojengwa sasa hivi haitaligusa, leo la Nyerere linaporomoshwa kama kibanda cha uganga kweli?

Mkasa huu ni wa usiku wa Septemba 20 mwaka huu, ambao sanamu hilo lenye uzito wa kilo 600 lilivunjwa bila mtu yeyote kusikia wala kuona na kusambaratishwa.

Yaani watu wasiojulikana sasa wamechoka watu wanaamua kuingia kwenye sanamu tena la mtu maarufu na mashuhuri wa Taifa hili, kweli?

Hii ni kasoro usiomithilika ya ulinzi wa kumbukumbu za Taifa hili.

Anasema Mzee Harun Mbeyu, Mwenyekiti wa Wazee wa Mkoa wa Tabora, kwamba ulishatolewa ushauri huko nyuma wa ulinzi wa sanamu hilo, lakini ukagonga ukuta wa masikio na kurudi. Hakuna utekelezaji!

Kwa mshangao mkubwa, Mzee Mbeyu anakaririwa akisema: "Hapa ndipo eneo Mwalimu Nyerere alihutubia na kutoa machozi akidai uhuru kutoka kwa Wakoloni na palifanyika mkutano huo baada ya kupigwa kura tatu za uamuzi wa busara wa kumwondoa mkoloni, hivyo pana historia kubwa sana ya harakati za ukonbozi wetu."

Wasiojulikana hao wanafanya machozi ya Mwalimu Nyerere yawe kama ya samaki majini, yaani yatoweke hivi hivi yasiwe na kumbukumbu adhimu kama hii! Walivunja na nini? Tingatinga au nyundo za kawaida? Hakuna ajuaye wala aliyesikia kishindo cha ubomoaji!

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha anayetoka mkoa mmoja na Mwalimu Nyerere, naye anasikika akisema: "Tunaweka mambo sawa, hapa pana historia ya ukombozi wa nchi hii na ni kielelezo na kumbukumbu muhimu, pia eneo la kujifunzia kujua harakati za Mwalimu Nyerere zilizofanyika hapa."

Akaahidi kuimarisha ulinzi na usalama na kuweka huduma ya umeme, kujenga majengo yote na kuimarisha miundombinu ya eneo hilo la kihistoria.

Sijaelewa kabisa, hasa nikizingatia kauli ya Mzee Mbeyu, ambaye alisema walishashauri huko nyuma, lakini hakuna utekelezaji.

Maana yake, kulisubiriwa mvua inyeshe paonekane wapi panavuja, lakini kuvuja kwake kumesababisha madhara ya kifikra na kiimani, hasa kutokana na upendo walionao Watanzania kwa kiongozi wao aliyetangulia mbele ya haki.

Najiuliza, hivi kama Mwalimu Nyerere amesikia kuwa sanamu la kumbukumbu yake limevunjwa na kuibwa viungo, anajisikiaje huko aliko?

Kwamba amesahaulika kiasi hiki mpaka hatua hii kuchukuliwa na wasiojulikana ambao ni kilio cha Taifa hili hivi sasa? Wametushinda, au?

Hivi kwanini viongozi wetu huwa wanasubiri la kutokea litokee ndipo wachukue hatua? Hivi kweli uongozi wa Tabora kwa maana ya serikali, haukuwa unajua uzito na umuhimu wa sanamu hili?

Jaribuni mtakapopata fursa mwende nchi za Scandinavia mwone na kujifunza, jinsi sanamu kama hizi zinavyoheshimiwa na kulindwa kama si kutunzwa.

Wizara yetu ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inajisikiaje kusikia au kuona sanamu la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Burito limevunjwa na wavunjaji wasiojulikana na kuondoka na shingo na fimbo yake?

Tusubiri uchunguzi. Kasinge Waitu Deo Alufonsi kwa kunifumbua macho na akili.

BIASHARA

# Pigo Uviko 19 China lilivyowafunza kinamama ubahili na bajeti kipato

**Na Mwandishi Wetu**

"Kila mwaka unapoisha, tulikuwa na pesa kidogo. Nilihisi kutokuwa salama lakini sikujua la kufanya," anasimulia Xiao Zhuo, mama wa watoto wawili mwenye umri wa miaka 36, mkazi wa jijini Xiamen, Kusini Mashariki mwa China.

Wakati wa janga la Uviko 19, Xiao Zhuo na mumewe walilazimika kuchukua mishahara iliyokatwa kwa asilimia 50. Likuwa pigo kubwa kwao kifamilia, alikuwa na mzigo pia wa kumtunza mama yake, aliyegunduliwa na saratani miaka mitano iliyopita.

Imekuwa mtindo kwa vijana wa Kichina kutafuta washirika wenye viwango sawa kiuchumi kwenye mtandao. Xiao Zhuo alitafuta ambao wana mitazamo sawa ya kuokoa pesa.

Toleo la kwanza la mfumo huo wa maisha ilianza Februari 2023 kwenye mtandao Instagram, ikavutia maoni milioni 1.7 na tangu wakati huo, ikawa ndio mtindo.

Wengi ni wanawake wenye umri kati ya 20 na 40, kinamama. Wengine wanasema wanataka akiba kwa ajili ya elimu ya watoto wao.

Baada ya kuvuka miaka yenye sera ngumu za maradhi ya ya Covid 19, ufufuaji uchumi China, unakabiliwa na gharama kubwa ya pango la majengo, kupungua bei ya bidhaa, kushuka uwekezaji kigeni na kuongezeka deni la serikali za mitaa.

"China, wanawake ndio huwa na jukumu la kugharamia nyumba kila siku. Kuona wanawake wengi wanaweka akiba ni kiashiria kwamba ukosefu wa ajira unaenea, sio tu miongoni mwa vijana," anasema Profesa Lu Xi, mtaalamu wa Sera za Umma, kutoka Chuo Kikuu cha Singapore.

Kuongezeka utashi wa watu binafsi kuweka akiba, kutafanya iwe vigumu zaidi kwa China kusawazisha uchumi wake. Katika miongo kadhaa iliyopita, ukuaji ulichochewa na uwekezaji katika miundombinu na nyumba za bei ya chini.

Na kadri uchumi wa China unavyokua, wataalamu wanasema kunakuwepo haja ya kuongeza matumizi ya ndani ili kuendeleza ukuaji.

Xiao Zhuo, anajihisi nafuu, anafanya kazi katika sekta ya Nishati safi, inayopanuka na inaripotiwa kuchangia asilimia 40 katika ukuaji uchumi wa nchi mwaka jana.

Anahisi analazimika kujiandaa kwa hatari, kwani wana familia na marafiki wanaopoteza kazi, wakiwamo wanaohudumia umma, kama vile hospitali na shule.

Mwezi Februari, Xiao Zhuo alijiunga na vikundi kadhaa vya kuweka pesa. Kila siku, wanachama wanapaswa kuweka bajeti na matumizi yao. Pia wanazuia kufanya manunuzi nje ya bajeti.

Xiao Zhuo anasema kajifunza mbinu za kuweka pesa, na mfano akajifunza programu ya sim inayomfanya kukokoa fedha China, kila siku kuokoa kuanzia Yuan moja hadi 183. Baada ya mwaka mmoja, ataweza kuwa na akiba ya karibu Yuan 34,000 na msukumo wa kufanya manunuzi kwa Xiao Zhuo umepungua.

Mwezi mmoja baada ya kupata washirika wa kuhifadhi pesa, amepunguza matumizi yake kwa asilimia 40, yakimpa matumaini ataokoa Yuan 100,000 baada ya mwaka - ongezeko mara kumi kutoka hapo awali.

Wanawake wengine, pia wanasema mbinu hiyo imewasaidia kuokoa pesa. Mwanachama mmoja anasema sasa anajipikia mwenyewe na amepunguza ununuzi usio wa lazima.

Mwingine anasema ameokoa zaidi kwa kujiweka bize kazini na atatafuta mambo mapya ya kumfurahisha ambavyo hayana gharama sana.

# SAMIA RASMI AIFANYA MBAMBABAY KUWA KARIAKOO

**INATOKA UK.11**

"Ushoroba huu ni wa barabara inayotoka Bandari ya Mtwara na inakuja kwa kilometa 822 mpaka bandari ya Mbamba Bay, ushoroba huu katika Kusini mwa Afrika, ndiyo ushoroba bora zaidi na mfupi kuliko shoroba nyingine zote," akasema.


Akafafanua ushoroba wa Mtwara umesheheni madini ya aina mbalimbali yakiwemo makaa ya mawe, dhahabu, uranium na madini mengine ambayo ni fursa kwa wakazi wa eneo lote la ushoroba.

Polepole akasema ni mbadala wa ushoraba wa Dar es Salaam hadi Lilongwe, ambao ni kilometa 1600, wakati ushoroba wa Mtwara ni kilometa 900.

Balozi Poleple akatoa ombi kwa mkoa Ruvuma, kuanzisha eneo maalum la kiuchumi linalowezesha kupatikana bidhaa zinazopatikana Kariakoo jijini Dar es Salaam, zipatikane Mbamba Bay.

Na ili kuhakikisha suala hilo linafanikiwa kwa asilimia 100, meli ya abiria ya Mbeya II ilitarajiwa kuanza safari za kuvuka ziwa kutoka Bandari ya Mbambabay Tanzania na kwenda nchini Malawi katika bandari za Nkatabay, Chilumba na Chipoka, ambako wangesafirishwa wafanyabiashara na mizigo kuja Mbamba Bay baada ya kuwa kituo cha kiuchumi.

Akasema, bidhaa hizo



Sehemu ya barabara ya Mbinga- Nyasa, ambayo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kaizindua juzi. **PICHA: MTANDAO**

zingeenda hadi Bandari ya Tete nchini Msumbiji, kupitia Ziwa Nyasa ambayo itakuwa ni fursa kubwa ya kibiashara.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma wakati huo, Kanali Laban Thomas, akaahidi mkoa umejiandaa kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji, hivi sasa bidhaa zote zitazohitajika, kupatikana bandarini Mbambabay, ili kupunguza umbali wa safari ya Dar es Salaam.

Ushoroba nyinginezo zilizopo kuuganan na ukanda hu oni za; Nakala Msumbiji mpaka Lilongwe Malawi, kilometa 995; Beira, Msumbiji hadi Lilongwe, kilometa 1022'; na ushoroba wa Durban, Afrika Kusini mpaka Lilongwe, kilometa 2,400.

**KAZI YA TANROADS**

Serikali kupitia Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS), nayo inaendelea na ujenzi wa barabara na madaraja mkoani Ruvuma, kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji wa watu na bidhaa

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Uongozi wa Mhe. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Miradi ya mikubwa ya Ujenzi wa Barabara, Madaraja na na Viwanja vya ndege, ikiwa ni pamoja na barabara ya Mbinga – Mbamba Bay kilomita 66.

Akizungumza Machi mwaka huu, Meneja wa TANROADS Mkoa wa Ruvuma, Salehe Mkwama, anasema serikali imejenga kwa kiwango cha lami katika Barabara ya Kitai -Lituhi - Ndumbi kilometa 95. 3; inayoelekea Bandari ya Ndumbi (Nyasa), itakayotumika kusafirisha makaa ya Mawe.

Pia, akataja mafanikio mengine ni kukamilika ujenzi wa Daraja la Ruhuhu lenye urefu wa mita 98.01, linalounganisha wilaya za Nyasa mkoani Ruvuma na wilaya ya Ludewa, mkoani Njombe.

Akasema, serikali ilikuwa mbioni kujenga upya barabara ya Songea – Makambako kilometa 295; nyinginginyeo inayounganisha Tanzania na Msumbiji, pia mkoa wa Ruvuma na Morogoro, kilomita 512.



## HABARI DODOMA

# Uongozi mpya CWT wawakosha wanachama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADHI ya walimu na wanachama wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) wameridhishwa na uongozi wa chama hicho kwa kuendesha shughuli zao kwa utulivu na kumaliza migogoro iliyosababisha mpasuko mkubwa ndani ya chama.

Walitoa pongezi hizo juzi wakati wakizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Mmoja wa walimu hao, James Minja alisema tangu Kaimu Katibu Mkuu wa CWT, Joseph Misalaba akabidhiwe ofisi Aprili mwaka huu, chama kimekuwa na utulivu mkubwa ambao umesaidia kurudisha imani kwa wanachama wengi.

Alisema kabla ya kuingia madarakani kwa Kaimu Katibu Mkuu huyo chama kilikuwa na migogoro mingi hali ambayo ilisababisha walimu na Watanzania kupoteza imani na CWT.

"Tangu kukabidhiwa ofisi kwa Kaimu Katibu Mkuu, Joseph Misalaba, kumekuwepo na utulivu mkubwa sana hali ambayo inatupa matumaini sisi walimu ambao ni wanachama tunaomba uongozi uendelee hivi ili kusaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu nchini," alisema Minja.

**"Tangu kukabidhiwa ofisi kwa Kaimu Katibu Mkuu, Joseph Misalaba, kumekuwepo na utulivu mkubwa sana hali ambayo inatupa matumaini sisi walimu ambao ni wanachama..."**

Aidha, alisema kutokana na utulivu ulipo sasa walimu wanapaswa kuwa kitu kimoja na kuwaunga mkono viongozi walipo madarakani ili kuendelea kurejesha hadhi ya chama ambayo ilianza kupotea.

"CWT ni chama kikubwa sana nchini lakini kutokana na migogoro, kesi na mambo mengine kilianza kupoteza hadhi yake na baadhi ya wanachama kukata tamaa lakini kwa mwenendo huu wa sasa na uongozi huu mimi siwezi kuondoka kamwe CWT.

Rai yangu kwa ambao waliondoka warudi kwani hiki ndicho chama kitakacho wasaidia siyo vinginevyo," alisema

Kadhalika, aliuomba uongozi huo pamoja na jitihada wanazofanya hivi sasa kutatua kero za walimu lakini pia wafanye ziara kwenye wilaya na mikoa kubaini changamoto ambazo bado hazijafanyiwa kazi.

"Huku wilayani bado wapo watu ambao wanakichafua chama kwa kufanya mambo ambayo hayana tija na walimu, hivyo tunaomba uongozi wa juu pia kuja huku wilayani kutoa semina ya namna ya kuhudumia wanachama," alisema.

Mwalimu Sailas Mgowela alimpongeza Kaimu Katibu Mkuu Misalaba kwa kuvunja makundi yaliyokuwapo ndani ya chama na kusababisha migogoro ya mara kwa mara.



Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dk. Federick Sagamiko akizungumza na wawakilishi wa vyama vya siasa na timu ya waratibu wa uchaguzi wa serikali za mitaa, jijini humo jana, wakati akitoa taarifa kuhusu ratiba za uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 27 mwaka huu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Dk. Gwajima asisitiza umuhimu bima ya afya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima amesema bima ya afya ni haki ya msingi ambayo inapaswa kupatikana kwa kila mwananchi.

Alisema hayo juzi wakati wa hafla ya matembezi iliyoandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ijulikanayo kama Bima Walk.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Janeth Mayanja, alisema elimu ya bima inapaswa kuendelea kutolewa kwa umma kutokana na umuhimu wake katika uthabiti wa uchumi wa nchi na ustawi wa jamii.

Alisema lengo la serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanapata bima kulinda afya na ustawi wao wa kifedha.

Kamishna wa Bima Tanzania, Dk. Baghayo Saqware, alisema matembezi hayo ni hatua muhimu ya kuendeleza juhudi za serikali za kuhakikisha kuwa raia wote wanapata bima ya afya.

Matembezi hayo yalihusisha wadau wa sekta ya bima na kutumia fursa hiyo kueleza umuhimu wa kuwa na bima miongoni mwa Watanzania kwa kuongeza elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Britam Insurance, Farai Dogo alisema wamejizatiti katika kukuza thamani ya bima ya afya ili watu wengi kupata huduma bora za afya.

# 'Vyama vya siasa vipendekeze wanawake kugombea uongozi'

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima ametoa wito kwa vyama vya siasa nchini kupendekeza majina ya wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye chaguzi za mitaa na mkuu mwakani.

Alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa uzinduzi wa mradi wa 'USAID wanawake Sasa' ambao pamoja na mambo mengine mradi huo unakusudia kuwajengea uwezo wanawake na wasichana waweze kushiriki kwenye nafasi za uongozi na michakato ya kidemokrasia, kuongeza uelewa kuhusu ukatili wa kijinsia na kuboresha asasi za kiraia.

"Tunaelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu, lakini pia tuna uchaguzi mkuu mwakani, tunaona namna wanawake wanavyojipambanua wanaweza kushika nafasi mbalimbali za uongozi, nitoe wito kwa vyama vya siasa wapendekeze wanawawake ambao wana sifa waweze kugombea nafasi mbalimbali za uongozi," alisema Waziri Gwajima.

Mradi huo wa USAID Wanawake Sasa wenye thamani ya shilingi bilioni nane utahusisha halmashauri saba za Tanzania Bara na wilaya nne za Zanzibar na utadumu kwa miaka mitatu, kwamba utajikita kuwanoa wanawake na wasichana kuwa na hari ya kushiriki kwenye siasa na michakato ya kidemokrasia.

Pamoja na mambo mengine mradi huo pia utahusisha kuwashirikisha wanaume kwenye majukwaa yao ili waweze kutambua nafasi ya wanawake kwenye siasa na uongozi.

# Serikali: Tutaendelea kudhibiti biashara ya punda

**Na Thobias Mwanakatwe,** DODOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema itaendelea kuchukua hatua za kudhibiti biashara haramu ya punda nchini kwa kuhakikisha wanahifadhiwa na kulindwa.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Edwin Mhede, alisema hayo jana wakati akifungua warsha ya uwasilishaji wa tathimini ya ustawi wa wanyama iliyofanyika mkoani hapa.

Alisema wanaoendelea na biashara ya punda watambue kwamba serikali haijalala bali itaendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha punda wanastawi.

Alisema ndiyo maana Oktoba Mosi 2022 serikali ilisitisha shughuli za kuchinja punda na biashara ya ununuzi wa ngozi ya mnyama huyo.

"Serikali inachukua hatua na itaendelea kuchukua suala hili kwa uzito unaostahili ili kuhakikisha punda wanahifadhiwa lakini pia kudhibiti biashara haramu inayowalenga punda," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa watu wanaokwenda kinyume na agizo la serikali kwa kuendeleza biashara hiyo, akisema watachukuliwa hatua kali.

Vilevile, alilipongeza shirika lisilo la kiserikali la Inades Formation Tanzania (IFTz) na Brooke East Africa na wadau wengine kwa kuwa mstari wa mbele kupambana katika kuhakikisha mnyama punda anaendelea kustawi hapa nchini.

Mkurugenzi wa Shirika la Inades, Mbarwa Kivuyo, alisema mradi wa kuboresha ustawi wa mnyama kazi punda ambao unatekelezwa katika mikoa ya Dodoma, Iringa na Singida umeanza kutekelezwa 2019.

Kivuyo alisema tangu umeanza kumekuwa na matokeo chanya kwa kufanikisha kusitisha biashara ya punda ambayo ilishamiri nchini kuanzia mwaka 2014 hadi 2022, hali iliyokuwa inahatarisha kupotea kwa mnyama huyo.



# Mradi wa maji mil.345/-kunufaisha wakazi 500

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WAKAZI 535 wa Kijiji cha Kiyogo Kata ya Masasi wilayani Ludewa mkoani wa Njombe wanatarajia kuondokana na adha ya kuliwa na mamba pamoja na kutembea umbali mrefu kufuata maji, baada ya serikali kuwachimbia kisima.

Hayo yalibainika juzi kwenye ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ludewa ya kukagua mradi wa maji wa Sh. milioni 346 unaotekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Baadhi ya wananchi hao akiwemo, Marieta Mahundi alisema walikuwa wanalala kwenye visima ili kupata maji ambayo pia yalikuwa ni machache.

Alisema walikuwa wanatembea zaidi ya saa mbili kufuata maji Mto Ruhuhu lakini wapo waliofariki kutokana na kuliwa na mamba.

"Maji shida kwa kweli wenzetu waliokuwa wanaenda mtoni (Mto Ruhuhu) kuchota maji walikuwa wanaliwa na mamba hadi watoto na sisi wenyewe," alisema Mahundi.

Mamerita Milinga alisema kabla ya mradi wa maji kuletwa kijijini kwao miaka ya nyuma wamepoteza ndugu wengi kwa kuliwa na mamba.

"Kwa kweli tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea mradi huu wa maji kwa sababu hatutaliwa tena na mamba," alisema Milinga.

Naye Kasimili Mahundi alisema walikuwa wanakumbana na adha kubwa ikiwemo kushindwa kufanya shughuli za kiuchumi.

**"Kwa kweli tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea mradi huu wa maji kwa sababu hatutaliwa tena na mamba," alisema Milinga.**

Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Ludewa, Mwita Isaya alisema mradi wa uchimaji kisima Kiyogo wenye thamani ya Sh. milioni 346 umefikia asilimia 78, unatarajia kuhudumia wananchi 535.

"Nipende kumshukuru Rais Samia Suluhu Hasan kwa kununua mitambo ya uchimbaji visima ambao umefanikisha kupata maji katika Kijiji cha Kiyogo kwa kuwa kijiji hiki kipo eneo ambalo hakukuwa na chanzo cha maji yanayopatikana juu ya ardhi," alisema Omari.

Mjumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Ludewa, Okolo Haule alisema kuwapo kwa mradi huo kutasaidia vijana kujiwekeza kwenye mradi wa kilimo cha umwagiliaji.

Mbunge wa Jimbo la Ludewa, Joseph Kamonga aliishukuru serikali kwa mradi huo akisema utasaidia kuwaweka salama wananchi hasa kinamama na watoto ambao walikuwa wakiliwa na mamba wakati wakienda kuchota maji mtoni.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Olivanus Thomas aliwataka wananchi kutunza mradi huo ili uweze kutumika muda mrefu kwa kizazi cha sasa na baadaye.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sunday Deogratius alisema mradi huo umekuja wakati sahihi kwa sababu utasaidia kupatikana kwa maji katika shule, zahanati pamoja na vituo vya kutolea huduma.



Fundi wa Kampuni ya ujenzi ya Bahaji, Wilson Meso akipiga plasta wakati wa ujenzi wa tangi la lita 200,000 la kukusanyia maji katika eneo la Nala, jijini Dodoma jana, mradi unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) wa uboreshaji wa upatikanaji wa maji katika eneo hilo, utakaogharimu Sh. bilioni 1.3 ulionza Julai 1, mwaka huu na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi sita. Mradi huo, utakaonufaisha wakazi zaidi ya 14,731, utahusisha ujenzi wa tangi, ulazaji wa mabomba kwa kilomita 7.8 na kusimika pampu mbili na uwekwaji wa mfumo wa kutibu maji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vitongoji 90 Njombe kupelekewa umeme

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 10 ili kutekeleza mradi wa umeme vijijini katika vitongoji 90 vya Mkoa wa Njombe.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa.

Alisema mradi huo umekuwa ukisubiriwa na wananchi mkoani hapa, hivyo ujio wa mkandarasi unapeleka matumaini ya kupata umeme kwenye vitongoji hivyo.

Alisema maeneo ambayo umeme huo utafika ni yale ambayo wabunge wenyewe wa Mkoa wa Njombe wameainisha wakiamini kuwa ni maeneo muhimu ili kuwakwamua wananchi kiuchumi.

"Hii ni awamu ya kufikisha umeme kwenye vitongoji niwatake wananchi wa Njombe wawe na mwitikio mzuri unapoona nyaya zinaletwa pale kwako au nguzo nawe unaweza kujiongeza ukavuta umeme kwako," alisema Omari.

Hata hivyo alimtaka mkandarasi wa mradi huo kumaliza mradi huo kwa haraka ili wananchi wafikiwe na huduma hiyo na waweze kutumia kwa shughuli zao mbalimbali.

Kaimu Meneja wa TANESCO Mkoa wa Njombe, Vaireth Mwinuka alisema Mkoa wa Njombe una vitongoji 1,840 lakini vitongoji 1,080 ndiyo vimefikiwa na umeme.

Alisema vitongoji ambavyo havijafikiwa na umeme kwa mkoa wote ni 756 ingawa upo mradi mwingine unaendelea wa ujazilizi na tayari mkandarasi amewasha vitongoji 80 na vimebaki 130.

"Tunamshuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupa vitongoji ili kupata umeme katika Mkoa wa Njombe na baada ya utekelezaji wa miradi yote mkoa utabaki na vitongoji 536 ambavyo havina umeme," alisema Mwinuka.

Mhandisi wa mradi wa REA Mkoa wa Njombe, Dunstan Kalugira alisema mkandarasi wa mradi huo alisaini mkataba na Wakala wa Umeme Vijiji Agosti 20, 2024 na anatakiwa kuanza kazi ndani ya siku 14 tangu aliposaini mkataba huo.

Mkandarasi wa mradi huo kutoka Kampuni ya China Railway (CRCERG), Palanivel Kandasamy alisema licha ya kuwa mradi huo ni wa miaka miwili lakini watahakikisha unakamilika kabla ya muda ambao wamekubaliana.

Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika aliishukuru serikali kwa kufanikisha mradi huo, akisema awali jambo hilo limekuwa likiwasumbua wabunge.

# 'Wakulima fanyeni utafiti wa soko kabla ya kulima'

**Na Elizabeth John,** WAG'ING'OMBE

WAKULIMA mkoani Njombe wametakiwa kufanya utafiti wa bei na soko la uhakika la mazao ambayo wanataka kulima kabla hawajaingia shambani, ili kujiepusha na hasara wanayoweza kuipata kutokana na kilimo cha mazoea.

Wito huo ulitolewa juzi na Ofisa Kilimo Mkoa wa Njombe, Stella Kutona wakati wa maonyesho ya Siku ya Mkulima ambayo yameratibiwa na Shirika la Maendeleo ya Kilimo Mkoa wa Njombe (NADO), yalifanyika katika Kijiji cha Igwachanya wilayani Wanging'ombe.

Kutona alisema ili mkulima aweze kulima kwa tija ni vema kabla ya kuanza kulima wafanye utafiti wa soko la zao ambalo wanataka kulima.

Aidha aliwataka wakulima kulima kilimo cha biashara badala ya kulima eneo kubwa bila kulihudumia, huku akisisitiza kutumia zana za kisasa.

Naye Ofisa Mazingira Mkoa wa Njombe, Gumbo Mvanda aliwataka wakulima kulima kilimo cha hifadhi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Pia aliwataka kutumia fursa za mikopo inayotolewa na halmashauri ili kupata mitaji ya kuendeshea shughuli zao za kilimo.

Kwa upande wake, Mratibu wa miradi kutoka Shirika la Maendeleo ya Kilimo Mkoa wa Njombe (NADO), Ernest Ng'umbi alisema lengo la maonyesho hayo ni kuwaunganisha wakulima na wadau mbalimbali ili kupata zana bora za kilimo na mbegu bora kuelekea msimu wa kilimo wa 2024/2025.

Alisema: "Katika msimu huu wa kilimo tunawashauri wakulima vitu vingi kwanza waone wataalamu wa kilimo ili waweze kufundishwa namna ya uzalishaji na kufuata kanuni bora, pamoja na kuunda vikundi ili wawe na sauti moja katika kununua pembejeo za kilimo zilizo bora"

Baadhi ya wakulima katika maonyesho hayo akiwemo Atukuzwe Mwendamseke alisema changamoto kubwa ambayo inawakabili kwa sasa ni ukosefu wa mitaji ili kufanya kilimo chenye tija.

Maonyesho hayo yameongozwa na kauli mbiu isemayo 'Harakati za kuboresha maisha ya sasa na ya baadaye kwa kutumia teknolojia, ubunifu bila kuathiri ikolojia kwa kilimo endelevu'.



# Idadi wanaokimbilia mikopo ya 'kausha damu' yawashtua wabunge

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wameitaka serikali kufanya tathmini kwa nini wananchi wanakimbilia mikopo yenye riba kubwa 'kausha damu'.

Walitoa agizo hilo juzi wakati wa kipindi cha maswali na majibu, kwamba walitaka kuchukuliwa hatua za haraka kutokomeza hali hiyo.

Mmoja wa wajumbe ambaye ni mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Ameir alisema mikopo hiyo imekuwa ikiwatesa wananchi na kusababisha baadhi yao kupokwa vitu vyao vya thamani baada ya kushindwa kufanya marejesho katika vikundi hivyo. Ameir alitaka kujua tofauti uliopo katika masharti ya kupata mikopo ya serikali kwa vikundi vya wajasiriamali na masharti yanayotolewa na mikopo ya kausha damu.

Alihoji kwanini wananchi wanaendelea kwenda katika mikopo hiyo badala ya kukopa katika mikopo inayotolewa na serikali ambayo ni nafuu na haina riba.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Riziki Pembe Juma, alisema sababu inayowasukuma wananchi kwenda kukopa ni kwamba kila mtu anamalengo yake na katika muda mwafaka.

Alisema mikopo ya serikali inayotolewa kupitia wakala wa uwezeshaji kuna taratibu ambazo zinahitaji kufuatwa lakini wananchi wanaona wanachelewa kufuata utaratibu huo.

Alisema hali hiyo huwalazimu wananchi kukimbilia katika mikopo yenye riba kubwa ambayo wanaamini kuwa wanaipata kwa urahisi.

Aidha, alisema tofauti kubwa kati ya masharti ya kupata mikopo inayotolewa na serikali kwa vikundi vya wajasiriamali na masharti yanayotolewa na mikopo ya kausha damu ni kwamba mikopo inayotolewa na serikali haina riba na marejesho yanafanyika kila mwezi.

> **Alihoji kwanini wananchi wanaendelea kwenda katika mikopo hiyo badala ya kukopa katika mikopo inayotolewa na serikali ambayo ni nafuu na haina riba.**

Alisema dhamana ya mikopo inayotolewa na serikali kwa vikundi vya wajasiriamali inatokana na wanachama wa vikundi vyenyewe, wakati mikopo ya kausha damu ni mali za wakopaji wenyewe.

Aidha, alikiri kuwa bado kuna wananchi walioomba mikopo inayotolewa na serikali kupitia mfuko wa uwezeshaji ambao bado hawajapata lakini pia wapo ambao wameshapata mikopo hiyo na tayari Sh. milioni 126.1 zimeshatumika kwa wananchi 254 Unguja na Pemba. Hivyo, aliwataka wananchi kuendelea kufuata utaratibu wa kuomba mikopo na wale ambao wameshakopeshwa kuendelea kufanya marejesho.



Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali (kulia), akijadiliana jambo na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Salha Mohammed Mwinjuma wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kampeni kukuza uchumi jumuishi yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kupanua huduma za kifedha jumuishi na wezeshi nchini wadau katika sekta ya mawasiliano wameelezea umuhimu wa kuanzisha huduma mbalimbali zitakazowezesha jamii kufanya miamala kupitia simu.

Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika kukuza uchumi jumuishi wadau hao wanasema kuna haja ya kuwa na kampeni maalumu itakayohamasisha jamii kutumia miamala ya simu katika maisha yao.

Katika kutambua hilo Watanzania watakaofanya malipo ya ving'amuzi, umeme na serikali watawezeshwa bonasi mbalimbali baada ya kuzinduliwa kwa promosheni iitwayo 'Jiboost'.

Kampeni hiyo inayoendeshwa na Airtel Tanzania inalenga kuwafikia Watanzania milioni 14 ambao ni wateja wao kwa mujibu wa Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Mkurugenzi wa Airtel Money, Andrew Rugamba, alisema: "Siku zote tumekuwa tukirahisisha maisha. Jiboost inakupa wepesi wa kufanya miamala pamoja na kurejeshewa fedha kwenye akaunti yako. Hii ni fursa kwetu sote ya kutunza na kupata fedha wakati tukiendelea kufanya matumizi. Najivunia kuwa sehemu ya mapinduzi haya".

Alisema kampeni hiyo inamruhusu mteja kuweza kupata supa bonasi ya Sh. 20,000 kupitia muamala unaotumwa kwenda kwa mtu mwingine, kununua muda wa maongezi, kununua vifurushi, malipo ya LUKU, malipo ya serikali na kununua vifurushi vya king'amuzi.

Mwezi uliopita, Tanzania ilizindua Mpango wa Kitaifa wa Ujumuishi wa Kifedha kwa mwaka 2023-2028, ambao unalenga kuongeza upatikanaji na matumizi ya bidhaa na huduma za kifedha za bei nafuu na ubora wa juu.

Tanzania ilipata mafanikio makubwa chini ya mfumo uliopita, ambapo idadi ya watu wazima wanaopata huduma za kifedha rasmi imeongezeka kutoka asilimia 86 mwaka 2017 hadi asilimia 89 mwaka 2023.

Kadhalika, matumizi ya huduma za kifedha rasmi yameongezeka kutoka asilimia 65 mwaka 2017 hadi asilimia 76 mwaka 2023.

# Serikali: Sukari ni bidhaa muhimu Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema miongoni mwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vilivyopo Zanzibar ni sukari ambayo ni moja kati ya bidhaa muhimu kwa wananchi.

Naibu Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Mudrik Ramadhan Soraga alisema hayo jana katika Baraza la Wawakilishi akijibu swali la Mwakilishi wa Wawi, Bakari Hamad Bakari aliyetaka kujua uwiano wa sukari inayozalishwa Zanzibar na iliyotoka nje.

Akijibu swali hilo, Mudrik alisema Zanzibar inatumia sukari inayoingizwa kutoka Brazil na India na inayozalishwa kutoka kiwanda cha Mahonda Kakskazini Unguja.

Alisema makadirio ya matumizi ya sukari Zanzibar ni wastani wa tani 36,000 kwa mwaka na Kiwanda cha Sukari Mahonda kinazalisha wastani wa tani 8,000 kwa mwaka sawa na asilimia 22 ya mahitaji Zanzibar.

Aidha, alisema kwa mwaka 2023, Zanzibar imeagiza sukari kutoka nje tani 31,402 na Kiwanda cha Mahonda kimezalisha tani 4,560 sawa na asilimia 14.5.

Alisema kwa kipindi cha Januari hadi Julai, 2024 uagizaji wa sukari kutoka nje ni tani 14,235 na tani 2,000 zilizozalishwa na Kiwanda cha Mahonda sawa na asilimia 14.

# Matukio ya udhalilishaji Z'bar yapungua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MATUKIO ya udhalilishaji wa kijinsia visiwani Zanzibar katika kipindi cha Agosti yamepungua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa kipindi cha Julai.

Mtakwimu wa Divisheni ya Takwimu za Jinsia na Ajira, Ramla Hassan Pandu, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema matukio 157 ndiyo yaliyoripotiwa katika kipindi cha Agosti mwaka huu kutoka matukio 165 yaliyoripotiwa Julai.

Ramla alisema licha ya kupungua kwa kasi hiyo ya matukio ya udhalilishaji kwa kipindi hicho lakini matukio ya kubaka yameripotiwa kuongezeka kwa kuwa na matukio 80 kutoka 68. Akitaja mchanganuo wa matukio hayo alisema kwa Agosti matukio ya kulawiti na kunajisi ni 14 wakati Julai yalikuwa 19, kuingilia kinyume na maumbile yalikuwa saba kutoka tisa kipindi cha Julai.

Alisema matukio ya kutorosha Agosti yalikuwa 16 kutoka 19 kipindi cha Julai, shambulio la aibu na kukashifu Agosti yalikuwa 24 wakati Julai ni 29 na shambulio la majeraha ni 16 kutoka 21 kipindi cha Julai.

Aidha alisema katika matukio hayo waathirika wengi ni watoto sawa na asilimia 87.2 ambapo wanawake ni asilimia 11.5 na wanaume asilima 1.3.

Alisema Wilaya ya Magharib A Unguja ndiyo inayoongoza kwa kuwa na matukio mengi ikilinganishwa na wilaya zingine, ikifuatiwa na Wilaya ya Magharib B ambayo.

Alisema matukio 117 kati ya 157 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 74.5, matukio 35 yapo Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Alisema katika waathirika 157 waliofanyiwa vitendo hivyo mmoja ni msichana mwenye ulemavu wa akili (15) ambaye alibakwa kisiwani Pemba.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARTHA LEKITONY** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo Bachelor Degree in Environmental Planning and Management chenye Registration namba **IRDP/BDEPM/17/0027** kilichotolewa na Institute of Rural Development Planning mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/LON/36133/2024.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MWITA P. ALPHONCE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0849-0130** kilichotolewa na **MOREMBE DAY SEC SCHOOL** mwaka 2006. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0109-0524** kilichotolewa na IHUNGO SEC SCHOOL mwaka 2009. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MOR/MOR/32416/2024.**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**EMMANUEL MUSSA MALULU** anatangaza kupotea kwa Result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S0784/0541** iliyotolewa na AIRWING SECONDARY SCHOOL mwaka 2024. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/203621/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEOFREY DONATH MNYAGATWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1601-0041 kilichotolewa na **TENGERU BOYS SECONDARY** Mwaka 2011. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0818-0577** kilichotolewa na TARAKEA HIGH SCHOOL mwaka 2014. Cheti cha Chuo chenye namba **BSESM 000376** kilichotolewa na Ardhi University mwaka 2018. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/208212/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ERICK ISACK MASEMO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0431/0033** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MTWANGO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/207835/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EDSON FRED KIBIKI** anatangaza kupotea kwa cheti cha Chuo chenye Registration No. **T/UDOM/2016/04195** kilichotolewa na Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na Transcript mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/MBA/29315/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARIA VICTORIA TIMBA,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha matokeo (Result slip) ya kidato cha sita **No ACS 026651.** Yeyote atakayeKiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa polisi:
**PHQ /DOD/DOD/RB/42638/2024.**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENT ACT**
**CAP 117**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**BY THIS DEED, I ENALA JACKSON NYIVAMBE** wholly absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former name **ENALA NYIVAMBE TWUPILILWE** and adopt as from the date of this poll and in substitution of the name **ENALA JACKSON NYIVAMBE** for purpose of evidence of such determination I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records, deeds documents and other writings and in all actions, suits and proceedings as well in all public and **ENALA JACKSON NYIVAMBE** hereby expressly authorize and require al and every person and whosoever at all times after the date hereof to designate, describe and address me by the name of **ENALA JACKSON NYIVAMBE** by the new name of **ENALA JACKSON NYIVAMBE** old **ENALA NYIVAMBE TWUPILILWE** and have set my hand at NJOMBE this 20 day of OCTOBER, 2022.
Dated at NJOMBE this 20 day of OCTOBER, 2022.

ENALA JACKSON NYIVAMBE is known to me personally in my presence this 20 day OCTOBER, 2022.

DEPONENT

BEFORE ME: M.M. KIDUGE
Signature ..........
Postal Address... 78 NJOMBE
Qualification... RESIDENT MAGISTRATE



## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SANLG WORLD WIDE INVESTMENT CO. LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 203 EKR.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/IRI/IRI/14647/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IGNATHIO ALLAN KYAMBILE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 532 ADV – ISUZU TRUCK** yenye Chassis namba **1621387.** Engine namba **780996.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/206268/2024.**

## KUPOTEA KWA LESENI NA KADI YA GARI

**LILIAN EMANUEL MASANCHE**

Anatangaza kupotelewa kwa leseni na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 714DMC,** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**PHQ/MOR/MOR/32318/2024**

## TAARIFA YA KUFUNGWA

INATAARIBIWA KUWA kutakuwa na Mkutano wa Mwisho wa Wanachama kwa madhumuni ya kuweka hesabu na kutoa maelezo yoyote kwa ajili ya kuhitimisha nambari ya usajili ya kampuni 121399, **GRAVITA VENTURES LIMITED,** siku 14 baada ya kuchapishwa kwa tangazo hili.

Mkutano utafanyika saa 4 asubuhi kupitia Teleconference siku ya kazi ambayo iko siku 14 baada ya kuchapishwa kwa ilani. Ajenda ya mkutano itakuwa ni kuweka hesabu na kutoa maelezo yake juu ya kufungwa kwa Kampuni.

Ikiwa mtu yeyote ana nia yoyote, anashauriwa kuwasiliana na kampuni kwa anwani iliyo hapa chini ndani ya siku 30 za notisi hii.

**Karimjee Attorneys**
**P.O. Box 76421**
**Dar es Salaam**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MSJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MAOMBI NA 22157 YA MWAKA 2024**

**GRACE MFINANGA..................................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**

Bi Grace Mfinanga amewasilisha maombi yake Mahakamani ya kutaka Mahakama itamke kuwa Ndugu **KEPHA PETER MWITI** ni marehemu baada ya kutoonekana na wala kutojulikana alipo kwa muda mrefu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 04 Mwezi wa kumi, 2024 saa tano asubuhi, siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya **Mh. Jaji S.D. MWAIPOPO.**

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 26 Mwezi wa tisa, 2024.

NAIBU MSAJILI

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA. 23700 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA CHARLES JEREMIA YONAZA..................MAREHEMU**

**SARAH RAPHAEL MKUFYA..................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 4 Mwezi OCTOBA, Mwaka 2024.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 25 Mwezi SEPTEMBA Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA

Principal Resident Magistrate I/c
Mwanga

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Tshisekedi: Rwanda iwekewe vikwazo

**NEW YORK,** Marekani

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) Felix Tshisekedi ametoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuiwekea Rwanda vikwazo kutokana na kuwaunga mkono waasi wa M23 wanaoendesha vita mashariki mwa nchi hiyo.

Rais Tshisekedi ametoa kauli hiyo wakati wa mkutano wa hadhara kuu ya Umoja wa Mataifa unaoendelea huko NewYork Marekani ambako viongozi mbalimbali wataendelea kuhutubia juu ya changamoto zinazoikabili dunia ikiwa ni pamoja na vita na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi.

Kiongozi huyo ambaye alitaka kuondolewa kwa wanajeshi wa Rwanda katika ardhi ya Congo, alisema uchokozi wa jirani yake unakiuka uhuru wa taifa hilo huku akisisitiza kuwa kuibuka tena kwa kundi la M23 kumesababisha mgogoro wa kibinadamu ambao haujawahi kushuhudiwa, na kwamba Rwanda inawajibika katika kuvuruga utulivu wa nchi hiyo.

**Zelensky alizinyooshea kidole China na Brazil huku akitilia mashaka maslahi ya nchi hizo ambazo zimekuwa zikiishinikiza Ukraine kufanya mazungumzo na Russia.**

Kwa miongo kadhaa sasa, eneo la mashariki mwa Congo lenye utajiri mkubwa wa madini limekuwa likishuhudia ghasia za makundi yenye silaha ambazo zimesababisha maafa makubwa.

Viongozi wengine wa Afrika waliohutubia jana ni pamoja na wa Ghana, Namibia, visiwa vya Ushelisheli, Libya na Madagascar. Wakifuatiwa na marais wa Malawi, Cameroon, Kenya, Burundi, Gabon, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Gambia, Lesotho, visiwa vya Comoros, Sudan na Sudan Kusini.

Miongoni mwa marais wengine waliohutubia usiku wa jana ni pamoja na wa Ufaransa Emmanuel Macron ambaye aliizungumzia mizozo ya Mashariki ya Kati pamoja na ule wa Ukraine.

Kuhusu mzozo unaoendelea kutokota kati ya Israel na kundi la Hezbollah la Lebanon, Macron alisema diplomasia ndiyo inayotakiwa kupewa kipaumbele katika kuutatua mzozo huo.

Rais huyo wa Ufaransa alikuwa kiongozi pekee wa nchi za Magharibi aliyefanya mazungumzo na rais wa Iran Massoud Pezeshkian na kumtaka kutumia ushawishi wake ili kuishinikiza Hezbollah kutouchochea mzozo huo.

Kuhusu vita vya Gaza, Macron alisema Israel ina haki ya kujilinda lakini mzozo huo umefikia pabaya huku akihimiza kufikiwa kwa makubaliano ya kusitisha vita, huku akitoa wito wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kufanyiwa mageuzi kuhusu mfumo wa matumizi ya kura ya turufu hasa yanapohusishwa matukio ya mauaji ya watu wengi.

Wakati wa hotuba yake, Macron aliiahidi Ukraine kuwa wataendelea kuipatia silaha inazozihitaji ili kujilinda na uvamizi wa Russia na kusema nchi yake inawaunga mkono raia wa Ukraine kwa ujasiri wao wa kukabiliana na Russia.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky ni miongoni mwa waliohutubia jana jioni na hotuba yake ilijikita katika kutafuta uungwaji mkono zaidi wa viongozi wa dunia pamoja na kuishutumu Russia kuwa inapanga mashambulizi dhidi ya vinu vyake vya nyuklia ambayo yanaweza kusababisha maafa makubwa.

Zelensky alisema Moscow imekuwa ikifanya ukaguzi wa vinu vya nyuklia vya Ukraine kwa kutumia satelaiti.

Zelensky alizinyooshea kidole China na Brazil huku akitilia mashaka maslahi ya nchi hizo ambazo zimekuwa zikiishinikiza Ukraine kufanya mazungumzo na Russia.

Waziri Mkuu wa Uingereza Keir Starmer, aliliambia baraza hilo kwamba Putin amekuwa akiwatuma raia wake kwenye kifo mithili ya kuwabwaga kwenye mashine ya kusagia nyama huku akihoji ni jinsi gani Russia inaweza kuonyesha uso wake katika makao makuu ya Umoja wa Mataifa. **DW**

## Putin apendekeza sheria kutumia nyuklia

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia Vladimir Putin amesema serikali yake inafikiria kubadilisha sheria na masharti ambayo Russia itayatumia ili kutumia zana zake za nyuklia dhidi ya mataifa anayopigana nayo vita.

Katika hotuba yake ya usiku wa kuamkia jana, Rais Putin, alisema Russia itachukulia shambulio kutoka katika taifa lisilo na silaha za nyuklia ambalo linaungwa mkono na taifa lenye silaha za nyuklia kuwa shambulio la pamoja, kauli inayoweza kuzingatiwa kuwa ni tishio la kutumia silaha za nyuklia katika vita vya Ukraine.

Ilielezwa kuwa Ukraine ni taifa lisilo na silaha za nyuklia ambalo linapata usaidizi wa kijeshi kutoka Marekani na nchi nyingine zenye silaha za nyuklia.

Pia ilielezwa kuwa kauli ya Rais Putin, inakuja wakati Kyiv inatafuta idhini ya kutumia makombora ya masafa marefu ya nchi za Magharibi dhidi ya maeneo ya kijeshi ndani ya Russia.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky alisafiri kwenda Marekani wiki hii na anatazamiwa kukutana na Rais Joe Biden mjini Washington, ambako ombi hilo la Kyiv linatarajiwa kuwa ajenda kuu.

Ukraine imeingia katika ardhi ya Russia mwaka huu na inataka kushambulia ngome ndani ya taifa hilo hasimu, ambazo ndizo zinatumika kurusha makombora nchini Ukraine. **BBC**




Wajumbe wa chama tawala nchini Uganda baada ya kuzindua kampendi ya kulinda kura za Rais Yoweri Museveni wakati wa uchaguzi ujao wa 2026. **PICHA: MTANDAO**

## Watu 145,000 kulinda kura za Museveni

**KAMPALA,** Uganda

CHAMA tawala nchini Uganda, cha 'National Resistance Movement' (NRM) kinatarajiwa kuajiri zaidi ya waganda 145,000 ili kulinda kura za Rais Yoweri Museveni katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka 2026.

Uamuzi huo unafuatia malalamiko ya Rais Museveni dhidi ya chama cha National Unity Platform (NUP) kuhusu wizi wa kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2021.

Museveni alisisitiza kuwa ana ushahidi wa kutosha kuhusu tuhuma dhidi ya NUP, juu ya kuiba kura.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kulinda kura za Rais Museveni, mshauri mwandamizi wa Rais wa nchi hiyo, Hadija Namyalo alisema kuwa NRM inalenga kuajiri watu wa kuanzia umri wa miaka 20 hadi 40.

"Tumekumbwa na changamoto wa kubadilishiwa kura zetu na ndio maana tumeanzisha kampeni hii, mahsusi kwa ajili ya uchaguzi mkuu ujao," alisema.

Naye, Makamu Mwenyekiti wa kwanza wa NRM Moses Kigongo, aliwataka waratibu wa kampeni hiyo kuepuka vitendo vya rushwa.

"Tunafahamu kuwa baadhi ya viongozi wamekuwa na tabia ya kuhonga mawakala wetu, tumejipanga kuhakikisha kuwa hilo halitokei katika uchaguzi ujao," alisema Kigongo. **TRT**

# JKT TANZANIA YAANZA MAJIGAMBO LIGI BARA

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya timu yake kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union hapo juzi, Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, amesema anataka kuona kikosi chake kinaimarika zaidi.

**Matokeo hayo ya juzi yameifanya JKT Tanzania kufikisha pointi sita baada ya kucheza mechi nne.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Ally, alisema anataka kuona kikosi chake kinacheza soka la ushindani katika kila mechi ili kusaka matokeo mazuri na kujiweka mahali salama kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kocha huyo alisema Ligi Kuu Tanzania Bara ni ngumu na ili timu yako ipate ushindi ni lazima wachezaji wapambane katika dakika zote za mchezo.

"Tunataka kuimarika zaidi, nataka kuwa na kikosi kinachocheza soka la ushindani, ni lazima tushindane ili kupata matokeo mazuri, tunatakiwa kujenga timu yenye hadhi ya juu, yenye kuogopewa.

Ili kufikia huko ni lazima tufanye jitihada zaidi, bila jitihada zaidi huwezi kufikia malengo," alisema kocha huyo.

Aliongeza ataendelea kukiimarisha kikosi chake kwa kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza kwenye mchezo wa juzi ili watakaposhuka tena dimbani wawe imara zaidi.

"Tunataka kucheza soka la kiwango bora, tutatumia muda mchache uliopo kufanyia kazi mapungufu, hatutaki kurudia makosa yaliyojitokeza huko nyuma, huu ni wakati wa mapambano na hatupaswi kuangalia nyuma, kikubwa ni kujipanga na mechi zinazofuata," Ally alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Coastal Union, Joseph Lazaro, alisema timu yake ilipoteza mchezo huo kwa sababu ya wachezaji kukosa utulivu.

Lazaro alisema wachezaji wake wameshindwa kutumia vyema nafasi walizotengeneza na kuzidiwa na wapinzani wao.

"Wenzetu wamepata nafasi wamezitumia, sisi hatukufanya hivyo, lakini tatizo lingine ni mabao ya mapema, unapofungwa mapema inaharibu mipango yako labda uwe na wachezaji wakubwa tu, tumeliona hilo, tunaenda kulifanyia kazi, ingawa ligi ndiyo inaenda hivyo," alisema kocha huyo ambaye timu yake imeamua kuhamia kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha.

Awali baada ya uwanja wake wa CCM Mkwakwani kuwa kwenye ukarabati, Coastal Union ilichagua kutumia Uwanja wa KMC ulioko Dar es Salaam.




Kipa wa Yanga Princess, Husna Mtunda akifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Ngao ya Jamii ya Wanawake dhidi ya Simba Queens itakayochezwa Oktoba 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# *Coastal Union sasa kuhamia Arusha*

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Coastal Union umesema rasmi timu yao inatarajia kuhamia kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha kwa ajili ya mechi zao za Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Uamuzi huo umekuja saa chache baada ya kupokea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa JKT Tanzania, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Isamuhyo.

Timu hiyo imecheza michezo mitano bila kupata ushindi wowote, ikiutumia Uwanja wa KMC Complex.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Omari Rajab, amesema wanatarajia kuondoka Dar es Salaam kutokana na suala la kimazingira ambalo kwa kiasi kikubwa ndilo linasababisha timu yao isifanye vizuri.

"Kwa sasa tunafikiria kuweka makazi Arusha, iwe ndiyo nyumbani kwetu na mechi zetu tutacheza huko. Nadhani tunapoteza mechi kwa masuala la kimazingira, timu yetu kwa sasa ipo katika wakati mgumu kidogo, mechi za nyumbani tunacheza ugenini, kwa hiyo hakuna hata mchezo mmoja msimu huu ambao tumecheza kwetu Tanga," alisema katibu huyo.

Aliongeza wamekutana na mazingira magumu ya kupata viwanja vya mazoezi Dar es Salaam na na umbali kutoka kambini kuelekea kwenye viwanja hivyo.

"Mazingira ni magumu katika jiji la Dar es Salaam kutokana na changamoto ya viwanja vya mazoezi, usafiri, umbali kutoka tunapokaa kambini kwenda mazoezini, hivyo tunaangalia kama tunaweza kukaa eneo ambalo timu inaweza kupata huduma za msingi na wakati sahihi," Rajab alisema.

# Kocha wa Biashara akaribia Pamba Jiji

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Biashara United inayoshiriki Ligi ya Championship, imetangaza kuvunja mkataba na kocha wake mkuu, Henry Mkanwa, anayedaiwa huenda akajiunga na Pamba Jiji ya Mwanza.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana pande hizo mbili zimefikia makubaliano ya kuvunja mkataba na klabu ikimtakia kila la heri katika majukumu yake mapya.

Kocha huyo ambaye alianza kufundisha Pamba Jiji Agosti Mosi, mwaka huu na kuiongoza Biashara United kwa mchezo mmoja dhidi ya Transit Camp, wiki iliyopita na kushinda bao 1-0, inadaiwa anatakiwa kwa udi na uvumba na Pamba Jiji ili kuchukua nafasi ya Mserbia, Goran Kopunovic aliyekalia kuti kavu.

Kocha huyo amekiri baada ya kutoka Musoma, kwa sasa yupo Mwanza kwa shughuli za kikazi, ambapo inadaiwa anarajiwa kukutana na mabosi wa Pamba Jiji, akiwamo Mkuu wa Mkoa, Said Mtanda kwa ajili ya kukamilisha mazungumzo na kusaini mkataba.

"Nipo Mwanza kwa sasa, nipo kwenye shughuli za kikazi hii hii ya mpira, nimeongea na Rais wa Biashara United akakubali ombi langu la kuvunja mkataba na sasa nina mazungumzo na timu nyingine huku," alisema kocha huyo.

Pamba Jiji, ambayo imepanda Ligi Kuu msimu huu haijashinda mchezo wowote kati ya mitano ambayo imecheza mpaka sasa, ikitoa sare nne na kupoteza mmoja.

Ilianza msimu kwa kutoka suluhu dhidi ya Prisons, kabla ya kupata sare nyingine dhidi ya Dodoma Jiji nyumbani kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza kabla ya kwenda kupata matokeo kama hayo ugenini dhidi ya Azam FC.

Baada ya hapo ikafungwa bao 1-0 nyumbani dhidi ya Singida Black Stars, kabla ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 pale pale, CCM Kirumba na Mashujaa FC kutoka Kigoma.

Ligi Kuu Tanzania Bara itaendelea tena leo kwa Fountain Gate kuikaribisha Kagera Sugar wakati kesho Namungo FC itawaalika Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RODRIGO KUMRITHI SALAH

LIVERPOOL ipo tayari kumnunua winga wa Real Madrid na Brazil, Rodrygo mwenye umri wa miaka 23, ikiwa mshambuliaji wa Misri,Mohamed Salah (32), ataamua kuondoka Anfield mwishoni mwa msimu huu. ***(Fichajes)***

### SARRI ANUKIA EVERTON

WAMILIKI wapya wa Everton, Friedkin Group wanataka kumleta kocha wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri, ambaye aliondoka Lazio Machi, kama mkufunzi wao mpya. ***(Corriere dello Sport)***

### VLAHOVIC, JUVENTUS KUTETA

JUVENTUS inatumaini kuongeza mkataba wa mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic,mwenye umri wa miaka 24 hadi mwaka 2028 au 2029, ingawa mazungumzo yanaripotiwa kukwama. Hivi karibuni Vlahovic amekuwa akihusishwa na Arsenal. ***(Calciomercato)***

### BRANTHWAITE ANUKIA UTD

KLABU ya Manchester United bado inamtaka beki wa Everton, Jarrad Branthwaite, 22, na watafanya jaribio lingine la kumsajili mchezaji huyo. ***(HITC)***

### FRIMPONG ATAJWA LIVER

BEKI wa Bayer Leverkusen na Uholanzi, Jeremie Frimpong, 23, anaongoza orodha ya Liverpool kuchukua nafasi ya Trent Alexander-Arnold, 25, ikiwa mchezaji huyo wa kimataifa wa England ataondoka katika klabu hiyo. ***(Football Insider)***

### CHELSEA YAMTAKA LUKEBA

CHELSEA inamnyatia beki wa RB Leipzig ya Ufaransa, Castello Lukeba, mwenye umri wa miaka 21, huku pia wakilenga kuwasajili wachezaji bora chipukizi duniani. ***(Teamtalk)***

### BONIFACE ANUKIA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Bayer Leverkusen na Nigeria, Victor Boniface, mwenye umri wa miaka 23 yuko katika orodha ya wamshambuliaji wapya wanaosakwa na Chelsea. ***(Teamtalk)***

### COSTA KUTUA BARCELONA

BARCELONA inamchukulia mlinda lango wa Porto wa Ureno, Diogo Costa mwenye umri wa miaka 25, kama chaguo la muda mrefu kuchukua nafasi ya kipa wa Ujerumani, Marc-Andre ter Stegen mwenye miaka 32. (***Mundo Deportivo*** )

### CASEMIRO, ERIKSEN KUTIMKA

KLABU ya Manchester United inataka kupunguza nafasi ya wachezaji wa safu ya kati na wanaweza kuwaachia Christian Eriksen na Casemiro, 32, kuondoka ifikapo Januari, mwakani. ***(Teamtalk)***

### CHELSEA YAMFUATA ONYEKA

KIUNGO wa kati wa Bayer Leverkusen Mjerumani Francis Onyeka mwenye miaka 17, anawindwa na Chelsea. (***Footbal Transfers)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG : WACHEZAJI HAWAKUJITUMA ZAIDI

**MANCHESTER,** England

Ni katika mechi dhidi ya FC Twente huku akilalamika walishindwa...

ERIK ten Hag amesema wachezaji wake hawakujitolea kwa asilimia 100 baada ya Manchester United kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya FC Twente kwenye mashindano ya Ligi ya Europa, juzi.

**United ilitangulia kwa bao la Christian Eriksen kipindi cha kwanza, lakini likasawazishwa kupitia Sam Lammers akitumia makosa ya Eriksen.**

Eriksen alisema baadaye FC Twente "walitaka zaidi" na tathmini iliyotolewa Ten Hag ilikubaliana na hilo.

"Ndiyo, uliona ni mchezo wa maisha yao," alisema Ten Hag.

"Walipigania kila sehemu na sisi hatukufanya hivyo kwa asilimia 100.

"Lazima uue mchezo, umalizaje, unatakiwa kufunga bao la pili halafu unaua mchezo.

"Tuna nia sana na unapokuwa nayo lazima ufanye, thibitisha ukweli. Hasa leo (juzi) katika kipindi cha pili tulikuwa tumeridhika sana.

Ten Hag alikatishwa tamaa hasa United hawakutumia nafasi zao zaidi. Safari ya kuelekea Crystal Palace siku ya Jumamosi iliisha kwa suluhu na licha ya kufanya majaribio 19 dhidi ya FC Twente, walipata bao moja pekee.

Kufumania nyavu kumekuwa tatizo msimu wote huku United ikifunga mabao matano pekee katika mechi tano za Ligi Kuu England.

"Lazima tulifanyie kazi hili," alisema Ten Hag. "Hilo pia ni wazi.

"Tuna wachezaji wa kutosha kwenye mstari wa mbele ambao wanaweza kufunga mabao."

HABARI MICHEZO

# MBAPPE MAJANGA MADRID



**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imetangaza mshambuliaji wake nyota wa kimataifa wa Ufaransa, Kylian Mbappe amepata majeraha na atakuwa nje kwa muda wa wiki tatu.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo kupitia tovuti yake rasmi imesema ripoti za kitabibu zimeonyesha Mbappe amepata maumivu ya misuli ya paja kwenye mguu wake wa kushoto.

Hivyo atakosa michezo kadhaa ikiwamo dabi ya Madrid dhidi ya Atletico Madrid, mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Lille na Real Valladolid.

Katika mchezo wa La Liga dhidi ya Deportivo Alaves Mbappe alionekana kuchechemea dakika chache kabla ya kutolewa na nafasi yake kuchukuliwa na Arda Guller dakika ya 80

Akiwa Madrid mshambuliaji huyo tayari amepachika mabao matano katika mechi saba za Ligi Kuu Hispania alizocheza.

# Son avunja ukimya mkataba mpya Spurs



**LONDON,** England

NAHODHA wa Tottenham Hotspur, Son Heung-min, amefichua bado hajafanya mazungumzo na klabu hiyo kuhusu mkataba wake unaomalizika.

Katika kikosi cha sasa, ni Ben Davies pekee aliyejiunga mwaka 2014, ambaye ametumia muda mwingi Spurs kuliko Son, ambaye hivi karibuni alisherehekea miaka tisa kwenye vitabu vya klabu hiyo.

Mkataba wa Son, ambaye ni raia wa Korea Kusini utaendelea hadi mwakani, ingawa inaaminika Tottenham wana chaguo kuanzisha kifungu cha nyongeza cha miezi 12.

Kocha Mkuu wa Spurs, Ange Postecoglou, alifichua mapema mwaka huu Son, ambaye ana umri wa miaka 32 alikuwa sehemu kubwa ya mipango yake kusonga mbele.

Katika mkutano na waandishi wa habari Son aliulizwa kama amefikia mwafaka na klabu hivi karibuni kujadili mkataba mpya.

"Bado hatujazungumza chochote," alisema Son.

"Ni wazi kabisa kutoka kwangu, ninazingatia sana msimu huu, kwa umri huu, kila sekunde haswa msimu huu, tuko kwenye mashindano mengi, nahisi kama ninajali zaidi juu ya hili.

"Kama ninavyosema, ninaangazia kikamilifu mwaka huu na ninataka tu kushinda kitu ambacho kila mtu katika klabu - wachezaji, pande zote - anastahili.

"Hilo ndilo ninalofanyia kazi. Katika siku zijazo huwezi kujua nini kitatokea, lakini nitatoa kila kitu kwa klabu hii kwa sababu imepita karibu miaka 10 na ninatoa kila kitu.

"Bado nina mkataba na klabu ambayo ni jambo muhimu sana na ninataka tu kutoa kila kitu hadi mkataba wangu utakapomalizika.

Kwa miaka kadhaa iliyopita, Son amekuwa akihusishwa na kuhamia Saudi Pro League, lakini anasisitiza nia yake ya kusalia Kaskazini mwa London.

# Scholes aelezea alivyomkera Ferguson

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Paul Scholes amefichua aliamini maisha yake ya soka yangefikia mwisho baada ya ugomvi wake na Kocha wa zamani wa timu hiyo, Sir Alex Ferguson mwaka 2001.

Scholes amesema hayo katika mahojiano maalum kwenye podcast ya mchezaji mwenzake wa zamani wa Manchester United, Nicky Butt inayofahamika kama Football's Greatest Eras.

Scholes amesema alikuwa na wakati mbaya baada kufanya kosa lililomkasirisha kocha huyo anayeheshimika zaidi kwenye ulimwengu wa soka.

Scholes alitokea benchi katika mchezo dhidi ya Newcastle United wakiwa nyuma kwa mabao 3-1 kisha wakapunguza moja lakini zikiwa zimesalia dakika 20 pekee kosa lake lilimfanya Alan Shearer kutanua uongozi kuwa magoli 4-2 katika mchezo huo wa msimu wa 2001/02.

"Aliniita na kunitukana sana, aliniita majina ya ajabu. Sijui nilipatwa na nini nikajikuta kwenye majibizano naye, unajua nina heshima sana mimi si mtu wa kujibizana na mtu kama Fergie lakini bila sababu yoyote nilijikuta namjibu"

"Aliniambia hutakaa ucheze tena kwenye hii timu, nikamwambia sijali. Baada ya mechi nilikaa kwenye basi usiku ule nikajisemea nimekwisha nadhani Jumatatu asubuhi nitasaini kwingine" alisema Scholes.



## HABARI MICHEZO

### Simba yamtaka Fei Toto CAF

INATOKA UK. 24

Ofisa huyo alisema kwa sasa akili na nguvu za viongozi wa klabu hiyo wamezielekeza katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyoko mbele yao baada ya kumalizika kwa mechi za kimataifa za CAF.

"Kwa sasa tumemaliza michezo ya kimataifa, tuna Ligi Kuu, masuala ya usajili umepita tayari na tutauzungumza pale utakapokuja tena mwezi Desemba, tutaona nani kaingia, kama Mpanzu au mwingine yoyote," alisema Ahmed.

Baada ya mechi ya jana usiku, Simba itarejea Tanzania Bara na kuelekea Dodoma kuwafuata wenyeji Dodoma Jiji FC kwa ajili ya mchezo mwingine wa Ligi Kuu utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani humo.

### Gamondi: Sokoine imetunyima mabao mengi

INATOKA UK. 24

kama walivyofanya leo (juzi), watakuwa bora sana," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Alionyesha furaha yake kwa beki wake, Bacca kwa kufunga bao la kwanza tangu ajiunge na Yanga.

"Nilichofurahi leo (juzi), ni beki wangu Bacca kufunga bao lake la kwanza tangu ajiunge na Yanga, na Shadrack Boka kuwa mchezaji bora ya mchezo, hii imenipa faraja sana katika mechi hii dhidi ya KenGold," Gamondi aliongeza.

Naye Kocha Mkuu wa KenGold, Jumanne Chale, alisema mbinu aliyowapa wachezaji wake kwa kiasi kikubwa ilifanya kazi, ingawa wamepoteza mchezo wa tano mfululizo katika ligi hiyo yenye timu 16.

"Nawapongeza Yanga kwa kushinda mechi hii, walinzi wangu walifanya kosa moja ambalo limetugharimu, wametufunga kutokana na uzoefu.

Mpira ni mbinu, yetu ilifanya kazi na tuliziba njia zote, ila kuna wakati walikuwa wanajisahau na Yanga wakafika langoni mwetu, nawapongeza sana vijana wangu wamefanya kazi kubwa sana, tumepoteza mechi ya tano mfululizo, lakini mchezo huu tumepoteza mbele ya timu kubwa, yenye wachezaji wenye ubora mkubwa, ilikuwa tusawazishe mwishoni, lakini wakati mwingine mpira ni bahati, hatukufanikiwa," alisema Chale.

Yanga imefikisha pointi sita ikishuka dimbani mara mbili wakati KenGold inaburuza mkia imecheza michezo mitano bila kuambulia pointi hata moja.

# FOUNTAIN GATE YATAMBA KUISULUBU KAGERA SUGAR

**Na Mwandishi Wetu**

LIGI Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea leo kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa uliokо Babati, mkoani Manyara kwa Fountain Gate kuikaribisha Kagera Sugar, huku wenyeji wakitamba wamewaandalia wageni kipigo.

Fountain Gate ambayo inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikikusanya pointi 10, itaingia uwanjani kucheza dhidi ya Kagera Sugar iliyopata ushindi wa kwanza Ijumaa iliyopita kwa kuwafunga KenGold mabao 2-0, baada ya michezo yake minne ya mwanzo kutoka patupu.

**Kocha wa magolikipa wa timu hiyo, Ally Mustapha 'Barthez', amesema wanatarajia kuendeleza walipoishia na kwa sababu wanacheza nyumbani.**

Barthez alisema hawataki kuwahuzunisha mashabiki wao ambao wamekuwa wakijitokeza kwa wingi kuwashangilia wanapocheza nyumbani.

"Tumejiandaa vizuri kabisa na mchezo huu, wachezaji wana morali baada ya kupata matokeo mazuri tukiwa ugenini dhidi ya Tabora United, hii imetupa nguvu kubwa sana chini ya mwalimu wetu mkuu, Mohamed Muya, kama kawaida yetu hatutaki kuwahuzumisha mashabiki wetu, huwa wanajitokeza uwanjani na kutushangilia sana na kuwapa wachezaji wetu nguvu kubwa," alisema Barthez.

Naye mchezaji tegemeo, Salum Kihimbwa, alisema siku zote timu hiyo huwa haina maneno mengi, badala yake wachezaji wanaiacha miguu iongee uwanjani.

"Siku zote Fountain Gate hatuna maneno mengi, hatuzungumzwi sana, lakini tunaacha miguu iongeee uwanjani, ila tunawaahidi mashabiki wetu tutaendelea kuwapa furaha, waje kwa wingi uwanjani" alisema Kihimbwa.

Timu hiyo imecheza michezo mitano, ikishinda mitatu, sare moja na imepoteza mechi moja tu ambayo ilikuwa ni ya kwanza kwao dhidi ya Simba, iliyochezwa Agosti 25 na kufungwa mabao 4-0, kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Paul Nkata, amesema baada ya kushinda mchezo wao wa kwanza, wachezaji wake wameanza kujiamini, ambapo licha ya kucheza ugenini dhidi ya Fountain Gate, lakini wana uhakika na ushindi.




Mashabiki wa Simba wakiwa wamebeba 'kapu na kibegi cha magoli' tayari kwa ajili ya kuingia kwenye Uwanja wa Amaan Complex, Zanzibar ili kuishangilia timu yao iliyokuwa inacheza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji, Azam FC jana usiku. **PICHA: MTANDAO**

# *Hosea Lugano achaguliwa tena Lindi*

**Na Somoe Ng'itu**

HOSEA Lugano amechaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Lindi (LIREFA), katika uchaguzi uliofanyika mkoani humo juzi.

Nafasi ya Makamu Mwenyekiti ilichukuliwa na Ahmedi Bongi wakati Rehule Nyaulawa alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

Kwa upande wa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya LIREFA walioshinda ni pamoja na Abdallah Kipingo, Ally Ally, Chande Kachele, Sharifa Mkwango na Juma Nandonde, ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa chama hicho.

Rais wa TFF, Wallace Karia, aliipongeza kamati hiyo ya utendaji iliyochaguliwa na kuwataka kusimamia maendeleo ya mpira wa miguu mkoani humo.

Karia ameutaka uongozi huo pia kutekeleza majukumu yao ambayo ni ustawi wa mpira wa miguu ndani ya mkoa huo.

Wakati huo huo, Blassy Kiondo, ametetea nafasi yake ya uenyekiti katika Chama cha Mpira wa Miguu cha Mkoa wa Rukwa (RUREFA).

Kanyinki Nsokolo alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti huku Ayubu Nyaulingo akishinda cheo cha Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa TFF na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ni Richard Ntinda, Goodhope Mushi na Sharifa Mangosongo.

# Michezo

Ijumaa Septemba 27, 2024

Nipashe




Ten Hag: Wachezaji hawakujituma UKURASA 21



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati waliokaa), akiwa na viongozi, makocha na wachezaji wa Simba walipomtembelea katika Ikulu ya Zanzibar juzi. **PICHA: SIMBA SC**

# SIMBA YAMTAKA FEI TOTO AFRIKA

## ●●● Inajipanga kumtoa Manula ili kufanikisha usajili huo kwa ajili ya...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikikamilisha mipango ya kumnasa winga, Elie Mpanzu, aliyemaliza mkataba na AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Simba inatajwa sasa imehamishia nguvu zake kumnasa kiungo wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto' huku ikimhusisha kipa, Aishi Manula 'Tanzania One'.

**Habari zilizopatikana jijini, Dar es Salaam zinasema Simba inataka kubadilishana wachezaji, ikijipanga kumwachia Manula aende Azam ili impate Fei Toto pamoja na fedha.**

Chanzo chetu kinadai Simba iko tayari kulipa kiasi cha Sh. milioni 350 katika kuhakikisha mchakato huo wa usajili unafanikiwa.

Taarifa zaidi zinasema Simba imeamua kutengeneza mtego huo kwa sababu ya mahitaji ya kila timu, ambapo wao wanamhitaji kwa udi na uvumba Fei Toto huku Azam FC ikitaka huduma ya Manula ili kufikia malengo.

Chanzo hicho kiliongeza tayari Simba imeanza mchakato wa usajili kutokana na kutinga hatua ya makundi katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, ambapo inaruhusiwa kufanya uhamisho, ingawa uhalali wake utaidhinishwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), wakati wa dirisha dogo la usajili.

"Mwanzo Azam ilileta barua Simba kumhitaji Manula kwa mkopo, lakini Simba ilikataa ikataka imnunue moja kwa moja, kwa maana hiyo mpaka sasa bado wanamhitaji, na viongozi wetu pia wanamhitaji sana Fei Toto, kwa maana hiyo wamekaa na kuamua kufanya usajili wa kubadilishana wachezaji na pesa juu.

Nadhani hili sasa linaweza kufanikiwa, tusubiri mwezi Desemba na Januari mambo yanaweza kubadilika kabisa, Manula akaenda Azam na Fei Toto akatua Simba," alisema mtoa taarifa huyo.

Simba inataka kuwaongeza Mpanzu kwenye eneo la winga na Fei Toto sehemu ya kiungo mshambuliaji ili kukiongezea nguvu kikosi chake, hayo yamesemwa na Rais na Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed Dewji 'Mo'.

Mwekezaji huyo amesema anataka kuona Simba inafika fainali au inatwaa ubingwa wa Kombe la Shirikisho Afrika, huku ikiwa ni maandalizi ya kuwa na kikosi imara kuelekea kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Mpanzu alikuwepo nchini hivi karibuni na alionekana katika mechi ya marudiano ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumapili iliyopita na Mnyama kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Al Ahli Tripoli kutoka Libya.

Fei Toto, katika mahojiano yake mara kwa mara amekuwa akisisitiza yeye ni mchezaji, anaweza kukipiga popote pale ambapo waajiri wake wa sasa Azam wataamua aende baada ya klabu hiyo kukamilisha uhamisho watakaokubaliana.

Naye Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kwa sasa dirisha la usajili limefungwa, hivyo masuala hayo yatazungumzwa itakapofika kipindi hicho.

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi: Sokoine imetunyima mabao

**Somoe Ng'itu na Adam Fungamwango**

LICHA ya kupata pointi tatu muhimu, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema ubovu wa Uwanja wa CCM Sokoine Mbeya ndiyo sababu iliyowanyima kupata ushindi 'mkubwa' katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya wenyeji KenGold iliyochezwa juzi jijini, Mbeya.

Mabingwa hao watetezi walipata ushindi wa bao 1-0, shukrani kwa beki wao, Ibrahim Hamad 'Bacca'.

Hata hivyo, Gamondi amewasifu pia wapinzani wao, KenGold waliocheza kwa nidhamu, akiitabiria makubwa timu hiyo kama wataendelea 'kukipiga' kama walivyofanya walipokutana nao.

Gamondi alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kufanikiwa kuondoka na pointi tatu ingawa waliamini watapata ushindi wenye idadi kubwa ya mabao.

"Kilichotuangusha ni uwanja, mpira ulikuwa hauwezi kutembea vile tunavyotaka, hauburuziki vizuri kwenye nyasi, tuliutawala mpira wa muda mrefu wa mchezo, tukapoteza nafasi nne kipindi cha kwanza, cha pili nadhani zilikuwa tatu, wao dakika za mwisho walipata nafasi nzuri lakini ilikuwa bahati kwetu, sasa tunahitaji kuboresha kiwango chetu, ingawa mpira wa miguu wakati mwingine huwa hivi," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema ilikuwa ni ngumu kucheza na kuifunga timu ambayo imetoka kupoteza michezo minne mfululizo.

"Ilikuwa ni ngumu kuifunga timu iliyopoteza michezo minne mfululizo, KenGold walicheza kwa nidhamu, kujituma na nguvu, walionekana kujipanga vyema kwa kufuata maelekezo ya walimu wao, naipongeza hii timu kama imeweza kucheza na sisi hivi na wakiendelea katika mechi zinazofuata kufanya

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >